**EATV** waingia ubia na AMREF maudhui vijana na wanawake
UKURASA 5




**MAHAKAMA** yaamuru watano kukamatwa kukaidi amri shtaka kuvaa isivyo heshima
UKURASA 7

**BOT** kuongeza akiba yake ya dhahabu nchini
UKURASA 5



**MOKWENA ATUPIWA 'VIRAGO' MAMELODI**
UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Julai 5, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581728

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Watoto pacha na njiti hatarini

**BINGWA** Muhimbili aanika tatizo lisilofahamika kwa wengi, atoa tahadhari... *Endelea ukurasa 3*






Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Neema Moshi (kulia), akimchunguza macho mwananchi aliyefika katika Banda la MNH kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Maprofesa watangaza dawa kudhibiti udanganyifu mitihani
UKURASA 2

UKURASA WA 5

### TUME YA MIPANGO YAHAKIKISHIA USIRI WATOA MAONI DIRA YA 2050

TUME ya Mipango imewahakikishia wananchi usiri katika maoni watakayoyatoa...



## Utafiti hali ya sekta ya habari nchini washtua
UKURASA 18

**MICHEZO** KOCHA FADLURAGHMAN ATUA NCHINI KUMALIZANA NA SIMBA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Maprofesa watangaza dawa ya kudhibiti udanganyifu mitihani

**Na Halfani Chusi**

MAPROFESA wa vyuo vikuu mbalimbali nchini wamependekeza njia za kudhibiti udanganyifu wa mitihani elimu za juu, kwa kuondoa utaratibu wa kuajiri kwa kutegemea vyeti pekee bali uelewa wakati wa usaili.

Aidha, wamependekeza kuwe na mfumo wa kumtambua mtahiniwa kwa alama za vidole kabla ya kuingia kwenye chumba cha mtihani, ili kuziba mianya ya wanaotoa fedha kufanyiwa mitihani.

Maprofesa hao walitoa mapendekezo hayo juzi katika kipindi cha mizani kinachorushwa na TBC kilichokuwa na mada ya 'Udanganyifu wa mitihani elimu ya juu'.

Makamu Mkuu Chuo Kikuu Huria Tanzaia, Prof. Elifasi Bisanda, alisema kupima uelewa kwa kutumia cheti ni njia inayochangia udanganyifu, ndio maana wanafunzi hupambana kwa njia haramu kupata vyeti na sio kuelimika.

Alitoa mfano wa Marekani ambayo imeshavuka hatua ya kumpima mtu kwa mtihani au cheti badala yake wanampima kwa kumhoji mpaka wanagundua kama atafaa kutumikia nafasi fulani au la.

"Tunahangaika bure mitihani sio kigezo halisi cha kupima uelewa wa mtu, fikiria unasoma mwaka mzima halafu unafanya mtihani kwa saa mbili unawezaje kutumia elimu ya mwaka mzima kuielezea kwa saa mbili?

"Tumekuwa wavivu kutafuta mbinu mbadala za kupima uelewa, nchi kama Marekani hawaangalii vyeti tofauti na huku, kule wenzetu wanakuhoji wanakuchunguza wanapokuhoji wanajua una uwezo kiasi na unaweza kuwafanyia kazi.

"Dhana ya mitihani kama ndio kigezo cha ubora wa elimu naielewa, lakini angalia mfano nchi kama Finland, ndio wanaoongoza kwa ubora wa elimu, lakini mtoto akianza darasa la kwanza hafanyi mtihani mpaka akifikisha miaka 16 ndio anafanya wa kuingia chuo kikuu na wote wanafaulu.

"Lakini elimu yetu kuanzia darasa la kwanza ni mitihani tu, Ninachofikiri wana taaluma tujikite katika kubuni namna gani ya kupima uelewa nje na kufanya mtihani.

Prof. Bisanda alifafanua namna aliowaita mamluki 17 kuingia katika chuo chake na kuwafanyia mtihani baadhi ya wanafunzi katika chuo hicho akibainisha kuwa walitumia njia ya kughushi vitambulisho.

"Baada ya kuwa tumebana kila njia ya udanganyifu, imeibuka hii mbinu ya kutafuta 'mamluki' wanakuja kufanya mtihani ukaanza huo ujanja, lakini kwa bahati nzuri tumekuwa macho wale wasimamizi walisaidia tukawanasa,' alibainisha.

Alisema walikuwapo wengine walitumia vitambulisho vinavyoonekana kama halali kumbe yale maandishi ya juu yalikuwa makubwa sasa wale wasimamizi walipoona vile hawakuwazuia kufanya mtihani utaratibu wetu ni muache kwanza tuone anataka kufanya nini.

Prof. Bisanda alisema walipoanza kufanya mtihani wakaguzi walipita kila dawati kukagua walipowafikia walibiani vitambulisho vyao vina shaka na kwamba kosa walilofanya ni la jinai watashughulikiwa na vyombo vya usalama kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema kipindi cha nyuma walilazimika kuondoa mitihani katika mikono ya walimu kwa kuwa wengi walihusika kuvujisha mitihani na kwamba kwa sasa wana mfumo unaoziba mwanya huo.

Katika kupambana na udanganyifu wa mitihani katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mhadhiri Mwandamizi wa Shule Kuu ya Elimu, Dk. Eugenia Kafanabo alisema wanakitengo cha udhibiti ubora kinachosimamia mfumo mzima wa ufundishaji kutoka utungaji wa mitihani, usahihishaji mpaka matokeo.

"Sio kwamba UDSM hatukosei, hapana wengi ambao wanakuwa na vitambulisho feki wanatengeneza mtaani kwa sababu hawajalipa ada, anakwenda kutengeneza ili aonekane ni mwanafunzi halali ilimradi afanye mtihani na wengine ndio kama hivyo wanatuma mamluki waje kuwafanyia mtihani.

"Kwahiyo siku hizi mwanafunzi anapokusanya mtihani tunalinganisha na kitambulisho chake kama namba ya mtihani aliyoandika inafanana na ya kwenye kitambulisho chake na wengi wanakamatwa kwa huu mfumo," alisema Dk. Eugenia.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Utafiti na Ushauri Elekezi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Razaki lokina, alisema udanganyifu upo katika ngazi zote za elimu.

"Udanganyifu wa mitihani ni vitu ambavyo vinafanana katika kila chuo, suala la vitambulisho tunajaribu kuona namna gani tunaweza kutumia mfumo wa sura ya mtahiniwa iwekwe katika mfumo," alisema.

Mtafiti wa Utahini na Udanganyifu Kwenye Mitihani, Dk. Setini Kita, alizitaja njia zinazotumika kwenye udanganyifu kuwa ni pamoja na kuingia na vikaratasi, kujiandika katika miili yao, kutumia majibu bila wasimamizi kujua, wafanyakazi kuvujisha mitihani, na kutumia simu.

**WANAFUNZI**

Mwanafunzi wa UDSM, Diniel Safar, akizungumzia udanganyifu wa mitihani alisema tabia hiyo inasababisha madhara kwa wasio na tabia hiyo kwa kuwa watashawishika kuingia kwenye mkumbo huo.

Mwanafunzi Rose Ngalo, alisema mpaka inatokea mwanafunzi anafanya udanganyifu huo maana yake kuna baadhi ya walimu wamehusika kwa namna moja ama nyingine," alisema.


KCBL Together, Transforming Lives

TANDAHIMBA COOPERATIVE BANK LIMITED TCBL "Our Bank for Our Development"

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KWANZA WA BENKI YA USHIRIKA TANZANIA**

TUNAPENDA KUWATAARIFU WANACHAMA NA WANAHISA KUWA MKUTANO MKUU WA KWANZA WA WANACHAMA NA WANAHISA WA BENKI YA USHIRIKA TANZANIA UTAFANYIKA KAMA IFUATAVYO:

| | | |
|---|---|---|
| TAREHE | : | 26 JULAI 2024 |
| SIKU | : | IJUMAA |
| MUDA | : | SAA 6.00 MCHANA |
| MAHALI | : | UKUMBI WA GENERATION ULIOPO JIJINI DODOMA MAENEO YA KISASA. |

TUNAPENDA KUWATAARIFU ZAIDI KUWA AJENDA ZA MKUTANO ZITASAMBAZWA KWA WANACHAMA NA WANAHISA SIKU SABA KABLA YA TAREHE YA MKUTANO.

KILA CHAMA/ TAASISI/KAMPUNI KITUME **MJUMBE MMOJA TU,** NA MWANAHISA BINAFSI ANAYO NAFASI YA KUHUDHURIA BINAFSI AU KUWAKILISHWA KWA MUJIBU WA MASHARTI YA BENKI.

KARIBUNI SANA,

Godfrey Ng'urah,
**KATIBU WA BODI - KCBL**

John Rugambo,
**KATIBU WA BODI - TCBL**

Tarehe: 04/07/2024


# Jamhuri yapewa nafasi ya mwisho kesi ya Malisa, Meya Jacob ifutwe

**Na Grace Gurisha**

MEYA wa zamani wa Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Boniface Jacob na Godlisten Malisa wamelalamika Upande wa Jamhuri kushindwa kuwasomea maelezo ya awali mara tatu mfululizo katika kesi inayowakabili ya kusambaza taarifa za uongo mtandaoni kwa lengo la kupotosha umma.

Washtakiwa hao wamedai kitendo hicho ni kuwasumbua kwa sababu sheria iko wazi kwamba upande wa mashtaka na polisi unatakiwa wafanye nini kabla kesi haijafikishwa mahakamani.

Malalamiko hayo waliyatoa jana mbele ya

Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kupita Wakili wao, Peter Kibatala wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo hayo.

Wakili wa Serikali Frank Michael alidai kuwa hawawezi kuendelea na PH (usikilizwaji wa awali) dhidi ya washtakiwa kwa kuwa jalada limeitishwa kwa ajili ya mapitio, hivyo wakaomba iahirishwe na wapangiwe tarehe nyingine.

"Hiyo PH inaahirishwa mara tatu mfululizo, sheria iko wazi kwa upande wa mashtaka na polisi kama watakuwa hawajakamilisha upelelezi, basi wasiwapeleke watuhumiwa mahakamani isipokuwa makosa makubwa, kwa sababu mapitio yalitakiwa yafanywe kabla ya kesi kuletwa mahakamani," alidai Kibatala.

Wakili huyo alidai kuwa kitendo hicho ni kusumbua washtakiwa, wanakwenda mahakamani lakini hakuna kinachoendelea. Akaoma mahakama itoe amri kwamba, kama itaridhia ahirisho hilo la Jamhuri, basi liwe la mwisho.

"Na kama siku itakayopangwa kesi haitoendelea basi nitatoa hoja kwamba washtakiwa waachiwe chini ya Kifungu Na. 226 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (CPA)," alidai Kibatala.

Baada ya kusikiliza hoja za kila upande, Hakimu Swalo alitoa maelekezo kuwa anatoa ahirisho la mwisho na pia ni kweli PH imeahirishwa mara tatu. Akaahirisha kesi hiyo hadi Julai 30 mwaka huu na kama upande wa Jamhuri hautaendelea siku hiyo, atafuata sheria kama inavyoelekeza.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu, likiwamo la kusambaza taarifa za uongo mtandaoni kwa lengo la kupotosha umma kuhusiana na kijana aliyedaiwa kupotea.

Ilidaiwa kuwa Aprili 22 mwaka huu, ndani ya Mkoa na Jiji la Dar es Salaam, mshtakiwa Jacob, kwa lengo la kupotosha umma, alisambaza taarifa ya uongo kupitia mfumo wa kompyuta wenye jina la Boniface Jacob @ExmayorUbungo wenye kichwa kilichosomeka 'wenye leseni ya kuua wameua tena'.

HABARI KITAIFA

# Hadhari yatolewa wazazi wa watoto njiti na pacha

## -Kundi hilo liko hatarini kukumbwa na...

Na Christina Mwakangale

BINGWA wa Magonjwa ya Macho Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Neema Moshi, ametoa angalizo kwa jamii, hasa kinamama wanaojifungua watoto chini ya wiki 34 (njiti) na pacha wawili au zaidi, kujihadhari na hatari ya watoto hao kukumbwa na upofu.

Bingwa huyo anasema watoto njiti, pacha zaidi ya wawili wanaozaliwa kabla ya miezi tisa kama ilivyo kibaiolojia, pazia lao la nyuma la kuonea (retina), huwa halijakamilika kuundwa, hivyo kuhitaji kuanza tiba siku 28 baada ya kuzaliwa.

Akizungumza na Nipashe katika Banda la MNH kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) jana, Dk. Neema alisisitiza kinamama kuhakikisha watoto waliozaliwa kabla ya wakati na pacha kufanya uchunguzi wa macho kuwaepusha na upofu.

Bingwa huyo alisema kuwa msimu huu wa Sabasaba, elimu wanayotoa kwa umma inagusa tatizo hilo, pia kukumbusha wasaidizi wa afya, wakunga kwamba kinamama wanaojifungua aina hiyo ya watoto, wafike kwa mtaalamu wa macho kufanyiwa uchunguzi.

"Upo upofu kwa watoto unaosababishwa na kuzaliwa kabla ya wakati au umri wa mimba kutimia au njiti wanaozaliwa chini ya wiki ya 34, mara nyingi pazia lao la kuonea, kitaalamu retina, huwa halijakomaa.

"Kwahiyo, inategemea kuna ambao pazia litakomaa bila kupata athari zozote, na wapo ambao litakomaa lakini kwa shida, asipotibiwa haraka, anaweza kupata upofu kwa maisha yake yote.

"Hivi sasa watoto wenye shida hizi kwanini tunawabaini kipindi hiki? Ni kwa sababu zamani watoto njiti waliozaliwa walikuwa ni nadra kupona kutokana na vifaa duni. Wengi wanaozaliwa hivi sasa wanapona na wanafikia umri mkubwa, vifaa vipo," alisema.

Bingwa huyo alieleza zaidi kuwa watoto hao hata kama wameruhusiwa kutoka hospitalini, wataendelea kuchunguzwa hadi wanapovuka wiki ambazo zilitakiwa wazaliwe, ili kuimarisha uwezo wa pazia la kuona.



Alitaja makundi ya walio hatarini kukumbwa na shida hiyo ni kwa waliozaliwa chini ya uzito mdogo zaidi usiovuka kilo mbili, mimba chini ya wiki 34 ambao huhitaji kuchunguzwa hadi pazia linapokomaa.

Bingwa huyo alisema kuwa katika kliniki ya macho Muhimbili, huwaona takribani watoto 10.

Dk. Neema alisema wengine walio katika hatari ya upofu ni watoto walio na shida ya upumuaji na wanaoongezewa damu kama vile pacha zaidi ya wawili, ambao mara nyingi huwa njiti; wana hatari ya kupata upofu wasipotibiwa.

"Tunashauri wakati daktari wa watoto anaendelea kuwachunguza, basi pia mtaalamu wa macho tushirikiane kuchunguza watoto hawa iwapo pazia lao liko sawa. Tiba ya tatizo hili ni pamoja na mionzi ya jicho na sindano.

"Akiendelea na tiba, ukuta utarejea na iwapo matibabu hayatafanyika katika wiki chini ya 34 anaweza akahitaji matibabu makubwa zaidi ya upasuaji kurudishia pazia ambalo huwa limejificha.

"Iwapo tiba itachelewa zaidi, hata hilo pazia linakuwa limeshaondoka hulipata tena, atakuwa na upofu maishani.

"Kama mtoto aliumwa sana akiwa njiti, baada ya siku 28 za kuzaliwa aonwe na mtaalamu wa macho. Hata kama mtoto yuko hospitalini na anapata msaada wa mashine ya oksijeni, lazima achunguzwe hili, ili kuwahi pazia lake kabla halijaondoka, pazia hujitengeneza kiasili kwa muda maalum," alisema Dk. Neema.

Bingwa huyo alisema kuwa hatua za ukuaji wa mtoto kutoka wiki ya kwanza hadi miezi tisa, ndiyo nguzo imara ya kila kiungo kinachounda mwili wake kwa kipindi maalum, hivyo wanaozaliwa chini ya wiki 34 ni rahisi kuwa na hitilafu kama vile retina kutokamilika kujitengeneza.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Mkumbo: Mamlaka zimegeuka polisi, zinavizia wafanyabiashara

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo (pichani), amesema Shirika la Viwango (TBS) na mamlaka nyingine zimegeuka kuwa polisi na kuwavizia wafanyabiashara badala ya kuwasaidia.

Aidha, amewataka watumishi wa mamlaka hizo kubadilika na kufuata mwongozo wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mkumbo aliyasema hayo jana mkoani Arusha wakati wa uzinduzi wa ofisi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) na awamu ya pili ya kampeni ya uhamasishaji uwekezaji wa ndani.

"Tunataka kuwa na mamlaka za urekebu kazi yake ni kuwawezesha wafanyabiashara kufanya kazi zao katika ubora unaotakiwa kama ni TBS jukumu lake moja ni kuhakikisha bidhaa ambazo zinatengenezwa Tanzania zina kiwango kizuri kisichohatarisha afya za watu wetu," alisema Mkumbo na kuongeza:

"Lakini bidhaa ambazo zinatengenezwa nchini na kupelekwa sehemu nyingine ziwe na vigezo vya kitaifa na kimataifa yaani bidhaa inayouzwa Tanzania unaweza kuiuza Kenya ama nchi nyingi ila hawa wenzetu sijui kama wapo hapa wamebadilika kuwa polisi badala ya kumsaidia mfanyabiashara afikie viwango vinavyotakiwa yeye amegeuka kuwa inspekta wanamvizia mfanyabiashara."

Mkumbo alisema mamlaka za serikali zinapaswa kuwezesha mfanyabiashara kuvuka hatua moja kwenda nyingine kwa kumshauri cha kufanya katika bidhaa yake ili iwe na ubora.

"Matokeo yake hizi taasisi zimekuwa ni TRA nyingine ya kukusanya mapato wapo bize kupambana na wafanyabiashara mwaka huu tunataka hizi TBS, Osha na nyingine tunawawekea mfumo ambao mfanyabiashara atalipa tozo mara moja, ili wao wakagawane sio mfanyabiashara azunguke mara aende Osha ama TBS," alisema Mkumbo.

Mkumbo alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameelekeza kufanya mabadiliko katika eneo hilo na tayari ameanza kulisimamia wanataka kuondoa utitiri wa leseni nyingi na iwe inatolewa moja inayojumuisha vitu vyote.

"Hatuna sababu ya kuwasumbua watu wetu kuzunguka kutafuta cheti kimoja baada ya kingine anatakiwa aende sehemu ya kulipia vyote na kupatiwa cheti na kuendelea kufanya biashara haya ni baadhi ya maeneo ambayo tunataka kuyashughulikia na Rais ameagiza," alisema Mkumbo.

Aidha, alisema serikali imejitahidi kuwekeza katika miundombinu ili waweze kusafirisha bidhaa zao kutoka eneo moja kwenda jingine.

Alisema kituo hicho kihakikishe kinatoa huduma bora kwa wawekezaji na kila wanachokihitaji wakipate katika eneo moja badala ya kupata usumbufu wa kuangaika kutafuta taasisi nyingine.

Aidha, Mkumbo alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kwa ubunifu na kasi aliyokuwa nayo katika kutekeleza maono ya serikali.



Awali, Makonda aliagiza wawekezaji wasichukuliwe kama maadui wanapokuwa wanafanyabiashara zao.

"Awe mwekezaji wa ndani ama nje ya nchi tusiwafanye kama maadui, tusiwaumize wawekezaji wetu kuna kipindi huwa nawaza itafika wakati tutaomba muongozo serikalini kabla ya mtu kuteuliwa tumuulize ulishawahi kufanya biashara gani iwe ni moja ya sifa," alisema Makonda.

Aidha, alisema mtu anatafuta mtaji ama kuuza kiwanja chake na kuanza biashara, wanapokuja watu wa serikali wawasaidie na sio kutafuta njia ya kuwahukumu ama kuwanyonga.

"Niombe kwenye hiki kituo cha uwekezaji ambacho mimi nina imani nacho kwa asilimia 100 watendaji wengine wa taasisi wanatakiwa kujua unalipwa mshahara kwa kodi za wafanyabiashara tuwahudumie vizuri na sio kuwaumiza," alisema Makonda.

Alisema anachokitamani ni kuona kituo hicho kinakuwa cha kwanza kwa ubora kwa Afrika kwa kutengeneza watalii wengi zaidi na kiwe na watumishi wenye weledi hawataki kuwa na watu wanaorudisha nyumba maendeleo ya uwekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, alisema uwepo wa kituo hicho mkoani Arusha kitasaidia wawekezaji kufungua miradi yao kwa haraka na kutoa mwanga kwenye uwekezaji wa kilimo, nyumba na kuongeza utalii.




KUMBUKUMBU



**Omukaile Ma Verdiana Kokuhirwa Saulo**
**(1938 – 2021)**

Leo tarehe 05 Julai 2024 imetimia miaka mitatu tangu kuondokewa na mpendwa wetu Omukaile Ma Verdiana Kokuhirwa Saulo Byemelwa. Kipindi cha miaka 3 kimekuwa kigumu sana kwa familia nzima ya Mzee Saulo Byemelwa, ndugu, jamaa na marafiki. Tulikupenda, tunakukumbuka, na tunakuombea upumzike kwa amani.

Tunapenda kuwaalika ndugu, marafiki na majirani kushiriki katika Ibada za shukrani na kumbukizi ya miaka mitatu ya kifo cha mpendwa wetu zitakazofanyika nyumbani Kataare – Kikukwe Kanyigo siku ya Jumamosi tarehe 6 Julai 2024 (Ibada ya Jumuiya ya Galilaya – kuanzia saa moja asubuhi) na siku ya Jumapili tarehe 7 Julai 2024 katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania - Usharika wa Kikukwe.

**Bwana alitoa na Bwana alitwaa, jina lake lihimidiwe.**

**Mama, Tutakukumbuka Daima!**



Mkurugenzi Mkazi wa AMREF Tanzania, Dk. Florence Temu (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Television (EATV) Ltd, Regina Mengi, wakitiliana saini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika ofisi za EATV, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana, ukilenga kutengeneza maudhui yanayohusu elimu ya afya, maji na usafi wa mazingira hasa kwa vijana na wanawake nchini. **PICHA: JOHN BADI**

# EATV, AMREF watia saini makubaliano maudhui ya elimu afya, maji, mazingira

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la AMREF Health Africa-Tanzania, limetia saini hati ya makubaliano na East Africa Television Limited (EATV) yakilenga kutengeneza maudhui yanayohusu elimu ya afya, maji na usafi wa mazingira hasa kwa vijana na wanawake nchini.

AMREF Tanzania ambao ni wadau wakubwa wa maendeleo wanaoshirikiana na serikali, wamefurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na East Africa TV, East Africa Radio na mitandao yake ya kijamii katika kuyafikia makundi mbalimbali ya watu hasa kundi kubwa la vijana.

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania iliripotiwa kuwa na vijana asilimia 77.

Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilifanyika kati ya Mkurugenzi Mkazi wa AMREF Tanzania, Dk. Florence Temu na Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Television Ltd, Regina Mengi, katika ofisi za EATV, Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Dk. Florence na ujumbe wake pia walitembelea vituo vya East Africa TV na East Africa Radio na kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa pamoja na uzalishaji wa vipindi vinavyoruka kila siku hewani.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Florence alisema wamejifunza mambo mengi katika ziara hiyo kwa kujionea vipindi mbalimbali vinavyotayarishwa.

"Ndio maana nilisema pale usione vinaelea vimeundwa, unaweza kusema mbona gharama za media kubwa, lakini nimeona uwekezaji uliofanywa si tu wa vifaa, hata aina ya watumishi mnaowahitaji ni wenye elimu zao na ujuzi.

"Nimefurahi wote ni Watanzania wanafanya kazi za viwango vya hali ya juu na mmetoa ajira kwa vijana, inahamasisha hasa mlivyoeleza mlikoanzia na mmeendelea kukua na kuikamata teknolojia, hii imetupa hamasa," alisema.

Dk. Florence alisema AMREF ni shirika lisilo la kiserikali na si la faida, lakini kinachofanyika kinaleta matokeo chanya ndani ya jamii.

"Tunashirikiana na serikali kwa karibu ikiwamo Wizara ya Afya, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na nyingine zinazohusika na jamii zikiwamo zinazojihusisha na mazingira, utendaji kazi wetu lengo kubwa ni kumfikia mwanajamii, na ngazi tunayopitia ni kinamama na vijana, hapo tunaunganisha mabinti na watoto," alifafanua.

Dk. Florence alisema wanapotembelea studio hizo na kukuta vipindi vya kinadada, kinamama na vijana, huku jamii nzima ikiangalia inaleta hamasa kubwa.

"Tunashukuru namna mnavyotupa ushirikiano, tukiwa na matukio ndani ya AMREF tunashirikiana na vyombo vyenu, na ninyi mnatushirikisha kwenye programu zenu mfano kampeni yenu ya Namthamini," alisema.

Alisema kupitia ushirikiano walioingia utaunganisha nguvu, ikiwamo katika kutafuta rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia.

"Ndio maana tunasema nguvu ya media ni kubwa, tunapotengeneza makala zinaweza kwenda mbali zaidi na tuna miradi yenye matokeo chanya mfano afya ya mama na mtoto, masuala ya mazingira safi, magonjwa ya maambukizi ikiwamo HIV na TB (Kifua Kikuu). Tunapokuwa na makala kama hizo watu wakiangalia wanapata mahali pa kujifunza," alisema.

Dk. Florence alisema vyombo vya habari ni muhimu katika afua za kiafya na katika kufikisha taarifa za mabadiliko ya tabia ya jamii ili kuwa na afya bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Television Limited, Regina alipongeza shirika hilo kwa kuchangua kufanya kazi na East Africa Television Ltd, kwa kuwa vyombo vyake vinawafikia watu wengi katika kuhabarisha na kuelimisha.

Aidha, alimhakikishia Mkurugenzi wa AMREF kuwa wapo tayari kuendelea kufanya kazi nao kufikisha ujumbe ambao umekusudiwa katika kuleta mabadiliko ya maisha ya kinamama na vijana.

Alisema wanaamini kwa ushirikiano wao watafikisha ujumbe mzuri zaidi kwa jamii kupitia makala na vipindi vinavyoruka katika kituo hicho.

"Bahati mbaya sana afya tunaiangalia baada ya kupata tatizo badala ya kuelimika na kujilinda na matatizo yanayoweza kutokea. Afya ya akili nayo tunaona imekuwa ni changamoto kubwa.

"EATV tunategemea tutajifunza mengi kutoka kwenu ya namna ya kuwakilisha na kufikisha ujumbe kwa jamii, tukiwa na nia ya kukuza na kulea jamii kwa ujumla ili iwe na afya bora na kuchangia katika ustawi wa jamii kwa ujumla," alisema Regina.

East Africa Television Ltd imeendelea kufungua milango ya ushirikiano na taasisi za kiserikali, zisizo za kiserikali, kampuni na wadau binafsi katika kutumia vyombo vyake vya East Africa Television, East Africa Radio na mitandao yake ya kijamii ili kuwafikia watu wengi zaidi hapa nchini katika kuwaelimisha na kuwahabarisha.

# BoT yajipanga kuongeza akiba ya dhahabu nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema katika mwaka huu wa fedha inatarajia kuwa na akiba ya dhahabu tani sita, kutoka kilo 418 za sasa, lengo likiwa ni kuongeza akiba ya fedha za kigeni.

Naibu Gavana wa BoT, anayeshughulikia Sera za Uchumi na Fedha, Dk. Yamungu Kayandabila, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitoa taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha ya Bodi ya Wakurugenzi wa BoT.

Kamati hiyo ilikutana juzi, pamoja na mambo mengine iliamua Riba ya Benki Kuu (CBR), kuendelea kuwa asilimia sita kwa robo mwaka itakayoishia Septemba 2024.

Dk. Kayandabila alisema hadi kufikia Machi, mwaka huu, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani bilioni tano kiasi ambacho kinakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi minne. Alisema upatikanaji wa fedha za kigeni uliimarika kiasi mwishoni mwa Juni, 2024 kutokana na ongezeko la fedha za kigeni kwenye mauzo ya tumbaku, dhahabu na shughuli za utalii.

Alisema matarajio ya BoT ni kuongezeka zaidi kwa fedha za kigeni nchini kupitia mapato yatokanayo na shughuli za utalii, mauzo ya madini, bidhaa za asili na usafirishaji wa chakula kwenda nchi jirani.

Alisema matarajio ya kuimarika kwa hali ya uchumi wa dunia na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia pia yatachangia ongezeko la fedha za kigeni hapa nchini.

"BoT inatarajia kuongeza akiba yake ya fedha za kigeni kupitia ununuzi wa dhahabu kutoka katika masoko ya ndani. Mpaka sasa akiba ya dhahabu haijaongezeka ipo kilo 418, lakini mwaka huu tunatarajia kununua hadi tani sita," alisema Dk. Kayandabila.

Kuhusu CRB, Dk. Kayandabila alisema: Kamati ya Sera ya Fedha ya Bodi ya Wakurugenzi wa BoT imeamua riba kuendelea kuwa asilimia sita kwa robo mwaka itakayoishia Septemba 2024."

Alisema tathmini ya kamati kuhusu mwelekeo wa uchumi na vihatarishi mbalimbali inaonesha kwamba utekelezaji wa sera ya fedha kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024 umefanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei na kubaki chini ya lengo la asilimia tano.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa Tanzania, Dk. Kayandabila alisema kamati ilibaini kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi nyingi kwa robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2024.

Alisema mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kuimarika kwa ukwasi katika masoko ya fedha duniani na Benki Kuu katika nchi nyingi kuanza kupunguza viwango vya riba.

"Bei ya mafuta ghafi ilipungua licha ya kuongezeka kidogo mwishoni mwa Juni, 2024. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu ikiashiria dhahabu kuendelea kutumika kama uwekezaji mbadala katika mazingira ya kushuka kwa thamani ya sarafu mbalimbali na migogoro ya kisiasa duniani."

# Tume ya Mipango yahakikishia usiri watoa maoni Dira ya 2050

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Mipango imewahakikishia wananchi usiri katika maoni watakayoyatoa kwa ajili ya kutengeneza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Laurence Mafuru, alisema hayo jana wakati wa kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Dira, kwenye kikao cha Wajumbe wa Tume ya Mipango, Timu ya Kuu ya Kitaalamu na Uandishi wa Dira ya Maendeleo 2050.

Aidha, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao katika mfumo tofauti uliowekwa, ili kuhakikisha kila mmoja anashiriki kutengeneza nyaraka hiyo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Wajumbe hao walikutana kwa ajili ya kupata picha kamili ya walipotoka na wanapokwenda katika kutengeneza dira hiyo, katika mkutano ulioongozwa na Prof. Mkumbo na kuhudhuriwa na wajumbe wake akiwamo Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba aliyehudhuria kama mjumbe.

"Na sisi kama tume pekee bila wizara hatuwezi kusonga mbele. Tumekutana ili kujadili kwa kina na kujiwekea mkakati na malengo ambayo si yakufikirika, lakini kutekelezeka," alisema.

Alisema wananchi wanaombwa kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao kwa kuzingatia vipengele vya dodoso, huku wakitakiwa kuongeza maelezo na taarifa za ziada ambazo ni muhimu kuzingatiwa katika Dira hiyo.

"Taarifa watakazotoa wananchi zitatumika katika maandalizi ya Dira na hivyo nawahakikishia usiri wa taarifa zao. Serikali inatambua kuwa, maono na maratajio ya Watanzania na mbinu za kuyafikia zinatokana na Watanzania wenyewe kupitia ushirikishwaji madhubuti katika maandalizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo," alisema.

Kwa mujibu wa Mafuru, ili kuhakikisha Dira hiyo inabeba maono na matarajio ya Watanzania kwa miaka 25 ijayo, ni muhimu wananchi na wadau wote wa maendeleo kushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa maandalizi ya Dira tangu hatua za awali hadi kukamilika kwake.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kongole Waziri Silaa kwa kuiweza Wizara ya Ardhi

**UUZAJI** viwanja holela kutoka kwa kampuni zinazonunua ardhi na kuwapimia wananchi, umewaingizia baadhi ya wanaonunua viwanja hivyo usumbufu mkubwa.

Kampuni hizo hutoa matangazo ya kuuza viwanja ambavyo mnunuzi huahidiwa kuwa na hati.

Kwa matangazo hayo wananchi wengi hushawishika kwenda kununua, lakini wakishalipa pesa, usumbufu huanza kutokana na kutopata hati walizoahidiwa na badala yake huanza kuhangaika kuzipata.

Hivi karibuni, Wizara ya Ardhi kupitia waziri wake, ilipiga marufuku matangazo yote ya kuuza viwanja bila kupata kibali kutoka wizara hiyo mpaka ivihakiki na kuruhusiwa.

Hiyo imetokana na baadhi ya viwanja hivyo kutoendana na vipimo vinavyotakiwa kisheria.

Ukipita barabara kuu nyingi jijini Dar es Salaam, utakutana na vipaza sauti vilivyowekwa barabarani vikitangaza ofa za viwanja.

Uuzaji huu holela wa kutumia vipaza sauti ambavyo muda wote vinapiga kelele barabarani pia ni uchafuzi wa mazingira kwa njia ya kelele.

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linapiga marufuku kelele katika maeneo ya umma kwa kuwa ni moja ya uchafuzi wa mazingira.

Hivyo, watu hao pia wanatakiwa wachukuliwe hatua kwa kubugudhi watu wengine.

Katika kudhibiti migogoro ya ardhi huko mkoani Pwani, serikali imezuia uuzaji wa maeneo katika Kitongoji cha Mbala, Kijiji cha Chamakweza Halmashauri ya Chalinze kutoa nafasi ya kupata mwafaka wa mmiliki halali wa eneo hilo ambalo lina mgogoro wa zaidi ya miaka 20 kati ya wakulima na wafugaji.

Amri ya kusitisha uuzaji wa maeneo hayo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge kwenye ziara ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Jerry Silaa, alipofika kusikiliza wananchi hao.

Kunenge alifikia kutoa amri hiyo kutokana na mgogoro huo huku kila upande ukidai ndio wakazi halali wa eneo hilo na kila upande ukimtuhumu mwingine kuwa mvamizi na kuuza maeneo kiholela.

Waziri Silaa aliahidi kutuma timu ya wataalamu kutoka wizarani kwa ajili ya kuhakiki mipaka ya vijiji na kutambua wakazi halali kijiji hicho.

"Nitaunda timu ya wataalamu kutoka wizarani kufanya uhakiki wa yaliyosemwa hapa tutafanya maamuzi ambayo hayataleta taharuki, tutakapofikia mwafaka tutatengeneza mpango wa matumizi bora ya ardhi na hii itasaidia kutatua migogoro inayotolewa."

Alielekeza viongozi wa vijiji kuzingatia Sheria namba tano ya Ardhi ambayo inatoa mamlaka ya ardhi kutolewa kwa kuzingatia taratibu zilizopo ikiwamo mikutano ya wananchi kwenye maeneo husika.

Wakati huo huo, Waziri Silaa amesema wizara yake imegawa Mkoa wa Pwani katika mikoa miwili ili kurahisisha utatuzi wa migogoro iliyopo kwa muda mrefu.

Wizara ya Ardhi, kupitia waziri wake pia imefanikiwa kutatua migogoro mingi ya ardhi kupitia kliniki zake ilizoanzisha katika wilaya mbalimbali.

Wananchi wengi ambao walikuwa wakisumbuka kupata hati, kupitia kliniki hizo wamefanikiwa kuzipata na waliokuwa na migogoro wamesuluhishwa na sasa wanaishi kwa amani.

Wizara nyingine zinapaswa kuiga mfano wa Wizara ya Ardhi ili kutatua matatizo yanayowakabili wananchi.

Waziri wa Ardhi alikuwa mstari wa mbele kusimamia kliniki hizo na kuhakikisha wananchi wanapata haki zao bila usumbufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



### Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

## Maofisa kata, mitaa tusijifungie ofisini, tutoke tukayaone haya

**NI** kawaida baadhi ya watendaji wa serikali kutumia nguvu kubwa yanapotokea majanga, magonjwa ya milipuko katika maeneo ya makazi ya watu nchini.

Ni kutokana na wengi wao kubweteka kwa kukaa ofisini, badala ya kwenda kwenye makazi ya wananchi.

Watendaji hao ninaowazungumzia ni waliopo kwenye ofisi za serikali za mitaa na kata za halmashauri za wilaya na miji nchini.

Watendaji hao wamekuwa wakikaa ofisini wasibiri kupelekewa kero na wananchi badala ya kwenda kwenye maeneo wanaokoishi kukagua hali halisi ya maisha.

Sana sana watendaji hao na wafanyakazi wao wakiwa wameongozana na polisi jamii wamekuwa wakionekana wanakwenda kwenye maeneo baada ya kupata taarifa kuna jambo ambalo linafanyika kinyume na taratibu na wanapofika wanageuka mahakama kwa kutoa hukumu ya papo kwa papo.

Hukumu hizo hutolewa kwa mtu ambaye amebainika kujenga bila ya kuwa na kibali, kutiririsha maji taka kwenye makazi ya watu yakiwamo kutoka kwenye choo kilichofurika, hivyo kutishia kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, matumbo na kuhara.

Maofisa hao wamekuwa ni wepesi kufika kwenye maeneo yao yenye mushkeli badala ya kwenda kukagua, kuelimisha wananchi madhara ya ujenzi holela na kutiririsha maji hayo machafu kwenye makazi na mitaro iliyopo barabara zinazounda mitaa hiyo.

Pamoja na kuwatoza faini kuanzia Sh. 100,000 na kuendelea, bado wanaotenda, watampa mlengwa muda wa kurekebisha dosari na bado atafikishwa kwenye mahakama zao za kata kujibu mashtaka.

Kero zote hizo, lawama zinatakiwa kuanzia kwa watendaji hao kwa kubweteka kwa kukaa ofisini, badala ya kwenda kwenye makazi ya watu kuwaelimisha athari za ujenzi holela wa makazi.

Ujenzi holela umekuwa ukisababisha kero nyingi za ukosefu wa barabara za mitaa, ambazo zingerahisisha mawasiliano kwa kuwa na usafiri wa uhakika wa vyombo vya moto wa kuingia na kutoka.

Kukosekana barabara, kumechangia wakazi wa maeneo hayo yaliyojengwa kiholela kukosa huduma ya ukusanyaji taka kwa magari ya kampuni za kandarasi za kuzoa taka kwa ajili ya kwenda kutupwa kwenye madampo yaliyotengwa na halmashauri husika.

Hilo limekuwa chanzo kwa makazi hayo kukithiri kwa uchafu kutokana na baadhi yao kugeuza njia za vichochoro wanakopita kurundika taka kwenye viloba.

Pia, maeneo hayo yanakosa huduma ya magari ya kunyonya maji taka baada ya vyoo kufurika, hivyo watu wanaoishi maeneo hayo kulazimika kutiririsha ovyo baada ya vyoo vyao kutapishwa na watu waliojiajiri kwa kazi hiyo.

Mara nyingi watu hao wamekuwa wakifurahia msimu wa mvua vyoo hivyo vinapofurika, kwa kubatiza kazi hayo hiyo kwa jina la 'kufokoa' bila ya kujali nao wanahatarisha maisha yao kutokana na kukosa vifaa vya kujikinga na magonjwa na dawa za kuua wadudu.

Shime maofisa watendaji kata, mitaa tuache kukaa ofisini kusuburi kuletewa malalamiko kutoka kwa wananchi kwani kunachangia kupalilia rushwa kutoka kwa baadhi yao wasiokuwa waadilifu.

Maofisa hao wawatumie watendaji wao wakiwamo wa idara ya afya, mazingira na usalama kwenda kwa wananchi kutoa elimu.

Hiyo itasaidia kudhibiti vitendo vya ukiukaji wa sheria za mipango miji ili nyumba zijengwe kwa mpangilio na kwa upande wa afya kutokomeza magonjwa ya milipuko na kuwa na jamii salama na yenye afya na furaha.

# Wafanyakazi kazi za ndani wanolewa kwenda kufanyakazi nje ya nchi

**Na Kulwa Mzee**

WIZARA ya Kazi na Ajira imewapa mafunzo ya kutambua na kuelewa mikataba ya kazi wafanyakazi wanaofanya kazi za usaidizi wa ndani wanaotarajia kwenda kufanya kazi nje ya nchi.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirika la Afya na Ustawi wa Jamii Afrika (COMHESWA), yalitolewa juzi na jana jijini Dar es Salaam.

Ofisa Kazi Mkuu kutoka Wizara ya Kazi, Rachel Magesa, alisema mfanyakazi wa ndani anapaswa kujua na kuelewa mkataba wake wa kazi na anayo haki ya kulipwa kiinua mgongo.

Alisema mfanyakazi wa ndani anayo haki ya mawasiliano, afuate maelekezo ya mwajiri kama hataki azungumze na simu muda wa kazi anatakiwa kuacha kufanya hivyo na anapomaliza kazi anaweza kufanya mawasiliano.

"Nyumba yoyote utakayokwenda ukanyimwa kabisa mawasiliano ni tatizo, mwajiri asizuie kuongea na simu saa 24, muda wa kazi uliopo kwenye mkataba uzingatiwe.

"Kabla ya kusafiri mnatakiwa kupima afya zenu, hamtakiwi kusafiri mkiwa na maradhi, hamruhusiwi kwenda na mimba ikitokea umesafiri ukifika unakokwenda utapimwa tena, ukikutwa na mimba utarejeshwa nchini," alisema.

Ofisa Kazi Mkuu, Eva Mangesho, alisema waarabu wanataka mfanyakazi apelekwe na wakala anayetambulika na serikali.

"Kila mfanyakazi lazima awe na mkataba halali, kubaki, apitie mafunzo kabla ya kusafiri.

"Tunatoa mafunzo ili kupunguza changamoto zinazotokea kwenye balozi zetu, balozi zimekuwa kama kituo cha polisi na kesi zingine hazina msingi," alisema.

Aliwakumbusha wanaposafiri hawaruhusiwi kubeba mzigo wa mtu kwa kuwa wengine ni wahalifu wanasafirisha dawa za kulevya.

Aliwaasa kuepuka kuwatumia mawakala wasiotambulika na Serikali.

Wakizungumza kwa masharti ya kutotajwa jina, mmoja wa wafanyakazi hao, alidai mishahara yao ni kuanzia Sh. 600,000 kuendelea na hawakatwi kodi.

Alisema mtu anaweza kutunza fedha hizo benki ambako ni mahala salama.

"Unaweza kutuma fedha nyumbani ukirudi baada ya miaka mitatu au miwili hukuti kitu ulichotarajia kufanya, ukitunza ndani mwajiri akijua anakopa na kurudisha inakuwa changamoto.

"Waajiri wametofautiana, wapo wenye moyo mzuri wa kukuelewesha inapotokea changamoto ya lugha, lakini wengine wakorofi, wanyanyasaji kwa kuwa tunaenda kufanya kazi tukafanye kazi na tuwaheshimu.

"Unaweza kuajiriwa katika nyumba yenye vijana, wanakushawishi kimapenzi, kataa fanyakazi, kuingia kwenye mahusiano ni kosa linaloweza kukufukuzisha kazi," alisema mfanyakazi mwingine ambaye hakupenda jina lake litajwe.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Masanja Kadogosya (kushoto), akifurahia jambo na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Jokate Mwegelo, wakati viongozi wa umoja huo kutoka mikoa yote nchini, walipofanya ziara katika mradi wa treni iendayokasi (SGR), kutoka Stesheni hadi Pugu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mahakama yaamuru watano kukamatwa kukaidi amri shtaka kuvaa isivyo heshima

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Sokoine Drive (Jiji), imetoa amri ya kukamatwa watu watano kati ya 18 katika kesi ya kufanya vitendo visivyo vya heshima kwenye sehemu za umma na kuvaa mavazi yasiyokubalika kwa nia ya kufanya ukahaba, kwa kushindwa kufika mahakamani bila taarifa.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi, Lugano Kasebele, wakati kesi hiyo ilipotajwa. Washtakiwa katika kesi hiyo ni Amina Ramadhani, Aisha Iddi, Mariana Sia, Mwajuma Hamza, Mariamu Hassan, Najma Hamisi, Sabrina Gabriel, Mariam Kitamoga na Elizabeth Michael.

Wengine ni Rosemary John, Recho Kindole, Lobi Daudi, Diana David, Jackline Daniel, Mwajuma Bakari, Jenifa John, Zainabu Hamisi na Recho Bakari. Hakimu Kasebele alifikia uamuzi huo, baada ya Wakili wa Serikali, Regina Kayuni kuwaita majina ili kujua kama washtakiwa wamefika mahakamani na kubaini kuwa watano hawakuwapo wakiwamo mshtakiwa namba mbili, saba, 11, 13 na 17.

"Kitendo hiki ni kutokuheshimu na kutotii amri ya mahakama na kuwa washtakiwa wanataka kufanya tabia hiyo kuwa ni mazoea, natoa amri ya kukamatwa kwa washtakiwa kushindwa kutii amri ya mahakama," alisema Hakimu Kasebele.

Wakili wa utetezi, Peter Madeleka alidai kuwa mahakama inaweza kuchukua hatua dhidi yao ili iwe funzo kwa wengine watakao onesha kutotii na kutofuata amri ya mahakama bila kujali mtu huyo ni nani na ana nafasi gani.


"Tumewaelekeza wateja wetu namna ya kutii na kufuata amri ya mahakama kwa jinsi tulivyoweza, kama mahakama inaona imevunja sheria basi ichukue hatua dhidi yao na wakamatwe," alidai Wakili Madeleka.

Hakimu Kasebele alitoa amri ya kukamatwa kwa washtakiwa hao watano ili iwe funzo kwa wengine watakaokiuka na kuacha kutii amri ya mahakama kama inavyowaelekeza.

Alisema kuwa kesi imepangwa kusikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Francis Mhina. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Julai 10, mwaka huu, kwa ajili ya washtakiwa kusomewa hoja za awali.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa Juni 14, 2024 katika maeneo ya Sinza Mori, Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote 18 walikutwa na tuhuma ya kujiweka katika namna ambayo sio sawa mbele za umma na kufanya vitendo visivyofaa na kuvaa mavazi yasiyokubalika kwa nia ya kufanya ukahaba.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# ‘Siri mafanikio NSSF ni uwekezaji sekta binafsi’

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba amefichua siri ya mafanikio ya NSSF kuwa yamechangiwa na serikali inavyohamasisha wawekezaji katika sekta binafsi, kuweka mazingira mazuri na kuwezesha kupata waajiri na wanachama wengi wapya katika sekta binafsi.

Mshomba alisema hayo alipotembelea banda la NSSF baada ya ufunguzi wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba yaliyobeba kaulimbiu: “Tanzania Sehemu Sahihi kwa Biashara na Uwekezaji.” Maonesho hayo yamefunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Filipe Nyusi, akisindikizwa na mwenyeji wake, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la NSSF, Mshomba alisema kwa mujibu wa taarifa za hesabu ambazo hazijakaguliwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, thamani ya NSSF kwa sasa inafikia trilioni 8.5 sawa na ongezeko la asilimia 77 ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita.

“Ongezeko hili ni kubwa hasa ukizingatia kuwa ndani ya miaka mitatu iliyopita ukuaji wa NSSF umekuwa mkubwa mno, hivyo tunampongeza sana Rais Dk. Samia kwa juhudi anazoweka kuhakikisha mazingira ya biashara hapa nchini yanakuwa mazuri ambayo yamechangia mafanikio haya,” alisema Mshomba.

Aidha, alisema wakati NSSF inaendelea kutekeleza mpango wake wa maendeleo unaoishia Juni 30, 2026, wanatarajia thamani ya Mfuko kufikia trilioni 11 ambayo itakuwa ni zaidi ya mara mbili ikilinganishwa na kipindi Rais Dk. Samia alipoingia madarakani.

Mshomba alisema kwa sasa NSSF imeelekeza nguvu ya kuwafikia wanachama wapya waliopo katika sekta isiyo rasmi ili waweze kujiunga na kuchangia katika NSSF kwa kuwa tayari wameshaweka mifumo mizuri ya usajili na uchangiaji pamoja na mafao yanayovutia kupitia Mpango wa Kitaifa wa Sekta Isiyo Rasmi.

Kuhusu ushiriki wa NSSF katika maonesho hayo, alisema ni kwa ajili ya kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa wanachama na wadau kuhusu huduma mbalimbali inazotoa mfuko huo zikiwamo usajili wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, uchangiaji, kulipa mafao, uwekezaji pamoja na uhakiki wa wastaafu.

Mshomba amesema pia wanatumia maonesho hayo kuwaeleza wanachama mambo makubwa ambayo NSSF imeyafanya kupitia huduma za TEHAMA na sasa wanachama wanaweza kujisajili kupitia lango la huduma binafsi kwa mwanachama na lango binafsi kwa mwajiri.

Alisema NSSF inaendelea kupata ushirikiano mkubwa kutoka serikalini na wataendelea kuboresha huduma zao mbalimbali.




Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kushoto), akimuhudumia mteja aliyefika katika banda la NSSF kupata huduma, kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yajipanga kuboresha vivutio misitu asilia

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abas, amesema serikali imejipanga kuboresha miundombinu katika vivutio kwenye hifadhi za misitu asilia ili kuvutia zaidi watalii katika eneo hilo.

Aidha, amesema kwa sasa kuna mwitikio mkubwa wa watalii wa ndani na nje kupendelea kutembelea vivutio vinavyopatikana katika hifadhi hizo asilia za misitu, na kwamba serikali imeona fursa katika eneo hilo na imejipanga kuendelea kuiweka katika mazingira ya mvuto zaidi ili yaendelee kutumika kuongeza idadi ya watalii.

Dk. Abas alitoa kauli hiyo jana alipotembelea banda la Wizara ya Maliasili na Utalii katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba, yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade).

Alisema uwapo wa miundombinu bora na mandhari nzuri kunawavutia watalii zaidi kupendelea kutumia muda wao mwingi katika misitu hiyo asilia.

Kadhalika, alisema wanaendelea kualika wawekezaji katika hifadhi hizo ikiwamo kujenga maeneo ya kisasa ya kupumzikia watalii, hoteli na huduma nyingine ambazo zitasaidia watalii kupata huduma zote wakati wakifanya utalii katika vivutio hivyo.

“Zamani watu walikuwa wanapendelea zaidi kwenda kufanya utalii wa kuangalia wanyama, lakini tunaona siku hizi mambo yamebadilika, kuna mwamko mkubwa wa kufanya utalii kwenye hifadhi zetu za misitu asilia, kwa mfano tunaona kule Pugu Kazimzumbwi, idadi ya watalii inazidi kuongezeka kila siku hata katika hifadhi zetu nyingine za misitu,” alisema Dk. Abas.

“Siku hizi tunaona watu wanaamua kwenda kupata hewa safi katika maeneo ya misitu yaliyohifadhiwa vizuri, hata kama kuna mambo yake yanamtatiza akienda kule akikaa baadaye anatoka yuko vizuri. Kwa hiyo sisi kama serikali tutaendelea kuwekeza na kuiboresha zaidi.”

Aliwaalika Watanzania kuwekeza katika ufugaji wa nyuki na uvunaji asali kwa kuwa nalo ni eneo jingine ambalo lina fursa kubwa kwa sasa.

Alisema kutokana na fursa zilizopo katika eneo hilo, serikali imewekeza nguvu zake ikiwamo kutoa ruzuku na kuwajengea uwezo wenye nia ya kuwekeza katika eneo hilo.

“Makundi mbalimbali wasisite kuchangamkia fursa zilizopo katika ufugaji wa nyuki na uvunaji wa asali kwa sababu hata soko lake liko vizuri,” alisema Dk. Abas.

# Rais Samia azihakikishia ushirikiano taasisi za dini

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi serikali itaendelea kushirikiana na taasisi za dini kujenga amani, umoja na ushirikiano nchini kwa manufaa ya wananchi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha salamu za pongezi kwa Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Mhashamu Wolfgang Pisa kwa niaba ya Rais Samia.

Alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi hizo katika kuchochea matokeo chanya kwa ustawi wa taifa.

“Tunashukuru tunapata ushauri, yapo mambo ambayo mnayafanya na kuiwezesha nchi hii iendelee, mshikamano wetu ndani ya nchi, umoja wetu ndio unaozaa utulivu na amani tuliyonayo,” alisema Majaliwa.

Alisema Rais Samia amesisitiza serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa baraza hilo na wako tayari kupokea ushauri kutoka kwao wakati wowote.

Alisema serikali itahakikisha ushirikiano huo hauishii kwenye ngazi za kitaifa tu bali utashuka hadi kwenye vitongoji, hivyo waendelee kuwa pamoja katika kuijenga jamii. “Wakati wote utakapokuwa na jambo ambalo unadhani serikali inahitaji kushauriwa, uwe huru na wakati wote unapoona kwamba unahitaji kuunganisha nguvu na serikali, sisi tutakupa ushirikiano,” alisema.

Askofu Pisa, alimshukuru Rais Samia kwa salamu za pongezi na kuahidi kuendelea kushirikiana na serikali kwa hali zote kujenga jamii iliyo bora.

Pisa ambaye ni Askofu wa Jimbo Katoliki Lindi, aliteuliwa kuwa rais wa baraza hilo Juni 21, mwaka huu, huku nafasi ya makamu wake akichaguliwa Askofu wa Jimbo la Katoliki Mpanda, Eusebius Nzingilwa.

Katika uchaguzi huo, baraza pia lilimchagua kwa awamu ya tatu Padri wa Jimbo Katoliki Singida, Charles Kitima kuendelea na nafasi ya Katibu Mkuu.

Wengine ni Padri Chesco Msanga, aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Askofu Mkuu Issack Amani, kuwa Mwenyekiti Kurugenzi ya Uchungaji na Askofu Eusebius Nzigilwa kuwa Mwenyekiti wa Kurugenzi ya Mawasiliano.

Pia wamo Askofu Augustine Shao katika nafasi ya Mwenyekiti Kurugenzi ya Ukaguzi na Askofu Henry Mchamungu katika nafasi ya Mwanasheria wa baraza hilo.



## HABARI KASKAZINI

# Bodaboda watuhumiwa kuua, polisi yawasaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

JESHI la Polisi mkoani Manyara, linawasaka madereva pikipiki katika Mji wa Babati wanaotuhumiwa kumuua kijana anayedaiwa kuhusika kula njama ya kuiba pikipiki.

Kijana huyo mwanaume anayehisiwa kuwa na miaka kati ya 20 hadi 25, alifariki dunia kwa kupigwa na kuchomwa moto na madereva bodaboda baada ya kudaiwa kushiriki wizi wa pikipiki akiwa na wenzake wawili waliotoroka.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), George Katabazi, akizungumza na Nipashe jana alisema bodaboda hao wanasakwa kwa kuhusika na tukio hilo. "Polisi tunawasaka vijana wa bodaboda waliohusika na mauaji ya kijana anayedaiwa kushiriki wizi wa pikipiki kwa kumpiga na kumchoma moto hadi kufa," alisema Katabazi.

Alisema tukio hilo limetokea Julai Mosi mwaka huu, majira ya saa 6:30 mchana, katika Mtaa wa Wang'warai Kata ya Babati, ambapo kijana aliyeuawa anadaiwa kula njama za kuiba pikipiki ya dereva aliyemkodi.

Hivyo, aliwakumbusha wakazi wa mkoa huo kuwa hakuna mtu aliyepo juu ya sheria bali wanapaswa kutoa taarifa ili polisi wafanye kazi yao na siyo wao kuchukua sheria mkononi.

"Endapo wangemfikisha Kituo cha Polisi huyo kijana badala ya kumuua tungeweza kumuhoji na akatueleza mtandao mzima wa wezi wa pikipiki walipo, kuliko kumpiga na kumchoma moto na kufa," alisema Katabazi.

Hata hivyo, alisema jeshi hilo linaendelea na operesheni ya kuwakamata watu wanaomiliki mali za wizi ikiwamo bodaboda.

"Raia wema wanapaswa kuendelea kutoa ushirikiano kwa polisi ili nasi tufanye kazi zetu kwa kutoa taarifa za wizi ambazo tutazichukulia hatua mara moja," alisema Katabazi. Mkazi wa Kitongoji cha Wang'waray, Ismail Bomboo, alisema tukio la watu kujichukulia sheria mkononi siyo zuri, kwani linapoteza ushahidi wa tukio na linaweza kutokea kwa asiye husika. Hata hivyo, alisema kuwa watu huchukua sheria mkononi baada ya kuona matukio mengi wezi hawafungwi jela ila wanaachiwa huru pindi wakifikishwa kwenye vyombo vya kutoa haki.



Mvuvi Mwarabu Mustapha (kushoto), akikabidhi vifaa vya uvuvi haramu kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani jijini Tanga jana, alipojisalimisha baada ya agizo la mkuu huyo, ambapo wavuvi 17 waliokuwa wakijihusisha na uvuvi haramu katika Mwambao wa Pwani ya Mwarongo, wamejisalimisha. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# RC ashtukia 'upigaji' ankara za maji, atoa agizo

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imeanza kuwabana watoa huduma za maji ngazi ya jamii kutumia mashine za kielektroniki, ili kuziba matobo yanayotokana na ujanja katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani, alisema matumizi ya mfumo wa utoaji ankara za maji kwa njia ya kielektroniki, kupitia mfumo wa malipo ya pamoja wa serikali una manufaa makubwa endapo utatumika ipasavyo.

Aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati akifunga mafunzo ya mfumo wa malipo ya pamoja wa serikali wa ankara za maji yaliyofanyika kwa siku 15, chini ya uratibu wa Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA).

"Uzuri wa mitandao una faida kubwa sana, hivyo twende tukaitue vizuri kwa kuitumia kwa kutoa huduma nzuri kwa watu wetu, kuna muda unaweza ukatuma ujumbe kumbe simu haipo hewani, hivyo kwa sasa tunavyoanza twende na vitu vyote viwili," alisema.Kuhusu taasisi za umma alisema: "Kwa maana kama mimi nikiamua kwenda kuishika eneo ambalo ni nje na makazi niliyopangiwa ni lazima nilipe. Hivyo, niwaombe wote waliopo kwenye taasisi ambazo wapo nje ya maeneo yao, tuwasaidie kulipa hizi bili ili isilete shida kwao katika ukusanyaji".

Meneja wa RUWASA, Mkoa wa Tanga, Upendo Lugongo, alisema watoa huduma hao wamepatiwa mafunzo, ambayo yanahusisha maduhuli ya ukusanyaji wa fedha katika sekta ya maji vijijini.

Kwa mujibu wa Lugongo, Mkoa wa Tanga una vyombo vya watoa huduma za maji vijijini 46, ambayo vyote vinafanya kazi.

"Mafunzo haya yanaenda kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli katika vyombo vya watumiaji wa maji, lakini kikubwa zaidi kuona fedha ambazo zinakusanywa ni sehemu ya fedha za serikali na zinatakiwa zisome kwenye mfuko wa serikali," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

### UNUNUZI WA MAHINDI NA MPUNGA KWA AJILI YA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2024/2025 KUANZIA TAREHE 10 JULAI, 2024

**1.0 Utangulizi**

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza. NFRA hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Ununuzi wa nafaka kwa mwaka 2024/2025 utaanza rasmi **tarehe 10 Julai, 2024.**

**2.0 Bei ya Kununulia Nafaka**

Bei ya kununulia mahindi itakuwa kati ya shilingi 500 kwa kilo hadi shilingi 600 kwa kilo, na mpunga utanunuliwa kwa bei isiyozidi shilingi 800 kwa kilo. Bei hizi zimezingatia tathmini ya bei za soko na gharama za uzalishaji katika maeneo ambayo NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa nafaka.

**3.0 Njia za Ununuzi Zitakazotumika**

i. Kutumia vituo vya ununuzi vitakavyofunguliwa nchini kote, ambavyo muuzaji yeyote anaweza kupeleka nafaka zake kuuza;
ii. Kutumia Vikundi vya Ushirika,Wakulima na Wafanyabiashara wakubwa wa mazao ambao wameingia makubaliano maalum na NFRA.
iii. Mikataba ya kuiuzia mahindi NFRA kwa waombaji wote waliokidhi vigezo imeanza kutolewa tangu tarehe 01 Julai 2024 kupitia Ofisi za Kanda na Makao Makuu, Dodoma. Waombaji wote wanahimizwa kuwasiliana au kutembelea Ofisi za Kanda walipowasilisha maombi yao ili kupata majibu ya maombi yao na kusaini mikataba kwa wale waliokidhi vigezo.

**4.0 Vituo vya Ununuzi**

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa ya Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa ya Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Singida), Arusha (Arusha na Manyara), Shinyanga (Mkoa wa Kigoma, Shinyanga na Tabora) na Kipawa (Morogoro na Tanga).

**5.0 Utaratibu wa Ununuzi**

Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima na Wafanyabiashara utafanyika kupitia mikataba maalumu ambayo Wakala unaratibu kwa kuzingatia maombi ambayo tayari yaliwasilishwa na Wadau mbalimbali kupitia Matangazo yaliyotolewa mwezi Machi, 2024.

**6.0 Utumiaji wa mizani ya kidigitali**

Kuanzia msimu huu wa ununuzi wa nafaka mwaka 2024/2025, NFRA itatumia mizani ya kidigitali katika vituo vyote vya ununuzi wa nafaka. Utaratibu huu utatumika katika vituo vyote vya ununuzi, kuhakikisha usahihi na uwazi katika vipimo vya nafaka zinazopokelewa. Hii itasaidia kuboresha ufanisi na kuondoa malalamiko yanayoweza kujitokeza katika upimaji.

**7.0 Utaratibu wa Malipo**

Malipo yote yatafanyika ndani ya siku 14 baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**

**04 Julai, 2024.**





# Mtatiro atoa angalizo mikopo 'kausha damu'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, amewataka wanawake wajasiriamali kuchukua tahadhari juu ya mikopo yenye riba kubwa 'kausha damu' ili wasijiingize katika umaskini.

Alitoa kauli hiyo katika ufunguzi wa Kituo cha Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kupitia uzalishaji wa sabuni za maji kutoka Shirika la Tanzanian Youth and Children (TYC).

Mtatiro aliwakilishwa na Ofisa Tarafa ya Shinyanga Mjini, Telezia Alois.

Pamoja na mambo mengine, aliwataka wanapokopa wawe makini na mikataba kwa kuangalia masharti ili wasijiingize kwenye mikopo hiyo.

"Nawasihi wanawake wajasiriamali ambao mmepewa mafunzo ya utengenezaji sabuni na shirika hili ambayo yatawakomboa kiuchumi tumieni fursa za mikopo ya halmashauri ya asilimia 10 ambayo itaanza kutolewa hivi karibuni na siyo hiyo ya mitaani," alisema Telezia.

Mkurugenzi wa Shirika la TYC, Lucas Daudi, alisema shirika hilo wapo kwenye utekelezaji wa mradi wa kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia uzalishaji wa sabuni, kwa ufadhili wa Tanzania Development Trust.

Alisema ndiyo maana wanawajengea wanawake ujuzi wa kutengeneza sabuni za maji ili wapate kipato na kuondokana na umaskini.

Mmoja wa wanawake waliopewa mafunzo hayo, Elizabeth William, aliahidi kutumia ujuzi huo ili kujiinua kiuchumi.



Baadhi ya wananchi wakiwa kwenye tope lililobubujika katika shamba la Musa Magagi, katika bonde la Nyankara, Kitongoji cha Pamila, Kata ya Matendo Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma juzi. **PICHA: ADELA MADYANE**

# Wadau waanika mikakati kuinua mapato Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WADAU wa maendeleo katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamebainisha mikakati mbalimbali itakayosaidia halmashauri kufikia au kuzidi makusanyo lengwa kwa mwaka 2024/25.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuweka kodi zote za uchimbaji dhahabu pale inapofika sokoni ili kuondoa mizunguko iliyopo kwa sasa. Aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti baada ya Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Halmashauri hiyo, Mang'era Marwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti 2023/2024 na uwekaji wa mikakati ya utekelezaji wa bajeti mpya ya 2024/2025 ili kuhakikisha wanafikia au kuzidi lengo la makusanyo.

Mchimbaji wa mgodi wa Ntambalale ulipo Kata ya Segese, Emmanuel John alisema ukusanyaji wa mapato wa ushuru wa mawe yanayosadikiwa kuwa na madini kwa kutumia mashine haisaidii halmashauri kupata mapato.

Alisema badala yake ni vema ukatumika mfumo wa kulipa kwa namba ya malipo (control number) kwani kinachokusanywa siyo kinachowasilishwa.

Pia, alisema ili kumwondolea mzigo mchimbaji na kuacha kukwepa kulipa kodi ni vema ushuru wa kifuko cha mawe wa Sh.1,000, kodi ya plant ya Sh. milioni 3.6 zikawekwa na kulipwa pamoja kwenye ushuru wa huduma kutoka asilimia 0.7 ya sasa mpaka asilimia moja.

Alisema hali hiyo inawapa manufaa wakusanyaji wa mapato kuliko serikali.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Samweli Mapula, alishauri kuanzishwa kwa kiwanda kidogo cha kutengeneza dripu mbalimbali ambazo zitauzwa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali jirani.

Alisema Hospitali ya Kolandoto ya Shinyanga inatengeneza dripu hizo na imesaidia kuongeza mapato ya hospitali na ufanisi wa kazi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hamisi Katimba alisema, ukosefu wa elimu ya kodi kwa wananchi ndiyo inayosababisha wengi kushindwa kulipa na kusababisha kukusanya nje ya bajeti iliyopangwa.

# MSD yataja chanzo ukosefu dawa hospitalini

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MENEJA wa Bohari ya Dawa (MSD), Kanda ya Kagera, Kalendero Masatu, amesema sababu kubwa ya ukosefu wa dawa na vifaa katika maeneo ya kutolea huduma za afya ni uwepo wa madeni ya muda mrefu, hasa kwa vituo vinavyohudumiwa na MSD.

Alisema sababu hiyo inaleta athari mbalimbali kwa wagonjwa na kurudisha nyuma hali ya kiutendaji katika vituo hivyo pamoja na MSD kutokana na madeni hayo kutokulipwa.

Aliyasema hayo juzi wakati akielezea hali ya makusanyo na mapato yanayotokana na uuzaji wa dawa na vifaa tiba, katika hospitali na vituo vya afya 478 kwa Mkoa wa Kagera na Geita inayounda kanda hiyo.

Masatu alisema ili bohari hiyo iweze kununua, kuuza na kutunza dawa na vifaa tiba, vituo vinavyokuwa vikifanyiwa huduma ya kupelekewa bidhaa vinatakiwa kufanya malipo kwa wakati ili na wao waweze kuboresha huduma kwa wateja wao.

Aidha, alisema kuanzia Julai, 2023 hadi Juni, 2024, mikoa hiyo imekuwa ikidaiwa Sh. bilioni sita Kagera wanadaiwa Sh.bilioni 4.8 na Geita Sh. bilioni 1.5.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Samwel Laizer, alisema tayari hatua za ulipaji zimeanza kufanyiwa kazi, kwamba vipo vituo vya afya vinavyofanya vikao juu ya namna gani wataweza kukamilisha deni la MSD.

Alisema hopsitali zimekuwa zikipokea huduma kwa haraka na kwa muda unaohitajika na kufanya huduma za dawa kwenye maduka ya hospitali kuwa asilimia 88.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Siima alisema ulipaji wa madeni utasaidia kuongeza na kufikisha huduma kwa wengine na MSD waweze kufanyia maboresho katika tiba na dawa.

# Wanawake 24 wafanyiwa upasuaji wa fistula

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

WANAWAKE 24 wanaokabiliwa na tatizo la ugonjwa wa fistula mkoani Shinyanga wamefanyiwa upasuaji bure.

Upasuaji huo ulifanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kupitia kambi ya madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake kutoka Hospitali ya Rufani Bugando jijini Mwanza, matibabu yaliyofadhiliwa na Shirika la Americares.

Mwakilishi kutoka shirika hilo, Dk. Jonas Kagwisage, alisema wana miaka 13 sasa wamekuwa wakitoa huduma hiyo ya matibabu bure ya ugonjwa wa fistula kwa wanawake kwa kushirikiana na madaktari bingwa wanawake kutoka Hospitali ya Rufani ya Bugando, sasa wamefanya kambi mkoani Shinyanga kutoa huduma hiyo.

Alisema katika Mkoa wa Shinyanga walianza kambi hiyo tangu Juni 23 mwaka huu, kwamba wamefanikiwa kuwafanyia upasuaji wanawake 24 na kuwarejesha katika hali zao za kawaida.

"Huduma hii ya matibabu ya ugonjwa wa fistula inatolewa bure, na shirika letu, ndiyo tuna gharamia kila kitu hadi chakula na nauli pia za kuwaleta hapa hospitali na tutawarudisha kwao," alisema Dk. Kagwisage.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake kutoka Hospitali ya Rufani Bugando jijini Mwanza, Dk. Elieza Chibwe, alisema tatizo la ugonjwa wa fistula bado ni kubwa sana kwa wanawake.

Alisema husababishwa na uchungu pingamizi kwa mwanamke anapokuwa mjamzito na hutokea tundu ambalo linaunganisha njia ya uzazi na sehemu ya haja kubwa na ndogo, na mgonjwa kusababisha kutokwa na haja kubwa na ndogo muda wote.

"Ugonjwa wa fistula ni wa aibu na matibabu yake ni upasuaji tu, na tunataka hadi kufikia mwaka 2030 tatizo hilo liwe limekwisha kabisa," alisema Dk. Chibwe.


Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. John Luzila, alishukuru kwa utolewaji wa tiba ya ugonjwa huo hospitalini hapo.



Ukurasa 12

1964 – MWAKA ULIOBEBA MZIZI WA MIPANGO MAENDELEO

Mapinduzi ya Mpango wa Kwanza Miaka Mitano, yalivyozalisha viwanda, SCOPO, Bwana Shamba...




Safari ya Korea na mauzauza yake-III

Ukurasa 13



## SAMIA NA HAMIENI MBADALA WA KUNI...

# EWURA CCC ilivyojitwisha jukumu la safari kutafuta mabadiliko yaliko

**Na Latifa Abdallah**

NISHATI safi ya kupikia ni nini? Unaweza kujiuliza swali hilo pale unapokutana na dhana hiyo masikioni kwako, kwa mujibu wa mwongozo wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 -2034) umeeleza, nishati safi ya kupikia ni dhana inayotumika kuelezea na kubainisha nishati na teknolojia sahihi ambapo kwa pamoja hutoa moshi wenye kiwango kidogo cha sumu pale zinapotumika kwa usahihi.

Dhana hii ina lengo la kuhakikisha usalama, uendelevu na urahisi wa upatikanaji wa nishati ya kupikia, kuokoa muda, pamoja na kupunguza gharama za matumizi, athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji.

Pia ni nyenzo muhimu katika kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa gesi joto.




Rais Samia Suluhu Hassan akipiga makofi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia) pamoja na Waziri wa Nchi, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, baada ya kuzindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwenye hafla iliyofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Mei 8, mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

Katika ufunguzi wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwenye hafla iliyofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Mei 8, 2024, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwataka Watanzania kuhama sasa kutoka kwenye matumizi ya mkaa na kuni kwa kupikia na kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ambayo ni gesi na umeme.

"Nawaomba Watanzania, mkakati wetu tukifika miaka 10, asilimia 80 tuwe kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Watanzania wote.

Mpaka sasa kwa takwimu zilizopo, asilimia 90 ya kaya zinatumia kuni na mkaa, jamani katika matumizi ya kuni na mkaa tunatumia miti mbalimbali, hivyo miti hiyo hutoa moshi mchanganyiko ambao unaleta madhara kwa watumiaji.

"Hivyo, Watu takribani 33,024 hupoteza maisha kwa mwaka kutokana na magonjwa ya mfumo wa upumuaji yanayosababishwa na uchafuzi wa hewa katika makazi.

"Mbali na uharibifu wa mazingira unaofanywa kutokana na matumizi ya shughuli za kibinadamu, ukataji wa misitu unachangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabia nchi.

"Inakadiriwa takribani hekta 469,000 za misitu hukatwa kila mwaka nchini. Ambapo nishati ya kuni na mkaa ndio chanzo cha uharibifu huo. Tubadilike Watanzania." Anasema Rais Samia.

Katika ufunguzi wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, Rais Samia alimwomba Waziri wa Nishati, Doto Biteko, kusimamia sera na mipango katika kuelimisha Watanzania sasa kwenye matumizi bora ya nishati safi ya kupikia.

Aidha, Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Nishati na Maji zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), linaendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji kila mkoa kuhusu matumizi sahihi ya nishati safi na maji, pia linaunga mkono mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Watanzania

Aidha, Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Nishati na Maji, Bi. Stella Lupimo, amesema, Baraza linafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wote wanapata elimu kuhusu nishati safi ya kupikia, kupitia kwa wajumbe wa kamati za watumiaji huduma za nishati na maji zilizopo katika mikoa yote ya Tanzania bara ili kuhakikisha wananchi wote wanaelimishwa kufikia lengo la mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Tunasisitiza utumiaji nishati safi ya kupikia uwe chachu ya maendeleo ya taifa letu, Watanzania waepuke matumizi ya nishati chafu (mkaa na kuni) ili kulinda mazingira, pia kuwaondoa kwenye hatari ya kupata maradhi ya kupumua kutokana na moshi wa kuni."

Matumizi ya nishati safi ya kupikia ni agenda mahusussi ambayo imechukua nafasi kubwa katika sera, mipango na mikakati ya serikali mbalimbali duniani. Umuhimu wa agenda hii unasukumwa na ongezeko la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

Aidha, Lengo Namba 7 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa limejikita katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, inayopatikana kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.

Hata hivyo, bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa nishati nafuu, endelevu na za uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali hususan ya kupikia

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

### 1964 – MWAKA ULIOBEBA MZIZI WA MIPANGO MAENDELEO

# Mapinduzi ya Mpango wa Kwanza Miaka Mitano, yalivyozalisha viwanda, SCOPO, Bwana Shamba...

**Na Peter Orwa**

WIKI iliyopita ilikuwa na sehemu ya simulizi Tanganyika mpya ilikotoka hadi kufika mwaka 1964, ikianza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu, iliyotimu mwaka 1964.

Mahudhurio yake alilenga sura kuu mbili, upande mmoja kubomoa misingi ya utawala wa kikoloni iliyokuwa na vikwazo katika matumizi ya rasilimali nchini mwao, mathalani fursa za kielimu.

Pia, ndani ya mpango huo, kukawekwa msingi ya mahitaji ya lazima yaliyoamuliwa kwa haraka, hasa katika matumizi ya mahitaji ya msingi kama vile afya, elimu, kilimo na matumizi ya ardhi.

Kutoka tafsiri pana, Tanganyika haikuwa koloni la kudumu na kwa maana hiyo, Wajerumani waliopokelewa baadaye na Waingereza hadi Uhuru, hawakuwekeza kwa kina, wakijua walikuwapo kipindi cha mpito.

Hiyo iliwafanya wawekeze katika mahitaji ya lazima, yaliyowawezesha kunufaika na nchi, ikiwamo uzalishaji malighafi mengi, yakiwamo kahawa na katani.

Mpaka Tanganyika inapata uhuru, kulikuwapo viwanda vichache na elimu shuleni inatolewa kwa ubaguzi, nafasi kubwa wakipata watoto wa Kizungu, kufuatiwa na Kiasia na Waafrika walipata nafasi kidogo, wengi wakibaki nyumbani.

Yote yalifanywa hadi Uhuru na miaka mitatu baadaye, nchi ikijipanga kujikwamua kutoka madhila ya ukoloni, sura kuu ya uchumi yaliyokuwa magumu kukosa huduma, sura ya uzalishaji kitaifa ikiwa "tunazalisha tusichokitumia na kutumia tusichozalisha."

**MAZITO YA 1964**


Ilipotimu mwaka 1964, Tanganyika ilifanya mageuzi makubwa ambayo mantiki na msingi yake hadi sasa, inabaki kuwa mithili ya katiba kuu kitaifa, jumla yako manne.

Mosi, ni kuundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayotokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa lugha rahisi, ikaundwa taifa imara zaidi kusalama, kijamii, siasa na uchumi, huku muundo wake ukibaki ni muungano wa kipekee kimataifa.

Pia, kuna kinachoenda karibu nayo ni kuundwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambalo lina historia kubwa katika kulinda nchi na ukombozi wa Afrika, ikibeba sifa hadi sasa weledi na uadilifu.

Eneo la tatu, penye sura kuu ya uchumi na maendeleo, ni pale Tanzania Bara ilipounda Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 1964 hadi 1965.

Hali kadhalika, uamuzi wa mwisho uligusa kuingiwa mfumo wa chama kimoja cha siasa, ikitafsiri aina ya kisiasa ya nchi, inayoangukia mlengo wa kushoto, itikadi ya kijamii, kitaifa kukitumika falfasa ya Ujamaa na Kujitegemea.



Tukio moja wapo la Azimio la Arusha lilivyokuwa.

Maudhui ya kiuchumi ya mpango huo miaka mitano, pia yaliegemea kusudio la kijamaa, mali na uchumi mkuu wa nchi kumilikiwa na serikali.

**MPANGO 1964-69**

Huo ndio ukawa msingi wa kidumu namna nchi iliendeshwa na miaka yote 50 hadi sasa, Tanzania yote inatumia muundo huo. Kwa kifupi, imebaki kama katiba ya kiuchumi na kisiasa kwa muungano wote.

Hata inapoingiwa kwa kina, urafiki wa viongozi wakuu Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Aman Karume, ulioanza hata kabla ya uhuru, mbinu na maudhui hayo ya 'bidhaa'za mpango huo, yalionekana Zanzibar kwa manufaa ya Wazanzibari.

Wakati huo, maendeleo ya nchi yakiwa changa na mambo mengi yako nyuma, Mpango wa Maendeleo 1964- 1969, ulilenga kuinua mambo ya msingi kwa Watanzania walioko katika maisha ya msingi.

Ni zama ambazo wastani wa asilimia 90 ya Watanzania walikuwa wakulima vijijini, maeneo ambako yalikuwa na huduma duni, ikiwamo miundombinu ya msingi kama vile barabara.

Wengi hawakupata kabisa fursa za elimu ya msingi, hali kama hiyo katika huduma za afya na ardhi. Huku mifumo yao ya kilimo na ufugaji, eneo ambalo limedumu hadi sasa kuwa nguzo ya uchumi wa nchini, baadhi yakiwa na majirani wa utalii nguzo nyingine ya uchumi na fedha za kigeni.

Katika utekelezaji wa mpango huo wa kwanza, Rais Nyerere, kwa kutumia mikakati ya ndani na nje, akaanzisha uwekezaji mkubwa kupitia mpango huo ulioazimia kuwapo muundo maaluma wa vijiji, nia ni kuunda huduma kama zahanati na shule za msingi, ambako ndio kulikuwa angalizo lake kuu.

Mtaji wa uwekezaji wake Rais Nyerere, alichukua sura kuu tatu. Kwanza kutumia mapato ndani ya nchi, kutafuta msaada wa kigeni, hasa nchi rafiki za kijamaa kama iliyokuwa Jamhuri ya Muugano wa Kisovieti (USSR) na China, ambayo ni marafiki kimaendeleo nchini hadi sasa.

Vilevile, tafsiri ya uendeshaji 'ujamaa halisi' ulitekelezwa mwaka 1967, ikatengenezea nchi mtaji zaidi mtaji wa maendeleo kupitia utaifishaji wa mali binafsi.

Ikipewa tafsiri kutoka tamko la chama - TANU kwamba "ni njia sahihi ya kuendesha taifa sawa na huru" kukishuhudiwa mali nyingi za umma kuzalishwa, ikiwamo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) iliyotokana na fedha ya kigeni.

Aidha, shirika la umma lililoitwa Msajili wa Majumba, majengo yake mengi yakiwa maghorofa mijini, makazi na ofisi yatokanayo na utaifishwaji wa Azimio la Arusha, yakaunda ajira na makazi mpya.

Ni zama ambazo misaada ilimiminika nchini na viwanda vingi kujengwa za kuzalisha mahitaji ya nchini, kufuta 'tunazalisha tusichoagiza na kuagiza tusichozalisha,' mathalan Dar es Salaam, ndio ukawa mzizi wa kumea viwanda katika Barabara ya Pugu (sasa Barabara Nyerere).

Vilevile, pengo kubwa la upatikanaji wa nguo nchini, kuwanusuru Watanzania na shida ya nguo, ghafla kunamea mipango na ushuhuda wa kujenga viwanda vya nguo kama Urafiki, ambao siri ya ujenzi wake mwishoni mwa miaka ya 1960, mtaji ulitokana na urafiki kati ya Tanzania na China.

Mengine ni majina kama; Tabotex (Tabora), Mutex (Musoma), na Kiltex ya Dar es Salaam, iliyoendana na kueneza umaarufu, utamaduni na siasa wa nchi katika vazi la khanga ukidhihirisha dhana ya wiki wiki iliyopita katika makala hii "Siasa na Uchumi na Uchumi ni Siasa."

Ndani ya mikakati hiyo na mipango tajwa ya kupanua viwanda, ikaunda nafasi mkutanua fursa za ajira nchini, ukitumika mfumo uliojulikana "Labour Intensive System," kwamba namna ya uzalishaji viwandani, mashine zinatumia nguvu kazi zaidi, tofauti na inayoitwa 'Capital Intensive," ikizama katika mashine.

Matokeo yake, ndani ya miaka hiyo mitano, kukaibuka kundi kubwa la wafanyakazi viwandani, huku serikali ikiajiri kwa kasi watumishi wa umma na wakati huo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), watumishi wake walianza kuingia mtaani.


Kilimo cha Ujamaa kikiendelea katika zama hizo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Kimsingi, katika miaka mitano kabla ya uhuru, kulikuwapo waajiriwa wachache sana wasomi katika utumishi wa serikali, huku walio na shahada za juu wanahesabiwa.

Katika kukabili hayo kwa haraka, ndani ya mlango huo wa kwanza, Rais Nyerere, akachukua juhudi kuanzisha vyuo vya utendaji kibiashara na kiutawala na ndio ikawa chanzo cha kuundwa kama Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Dar es Salaam.

Nako katika uzalishaji malighafi nma ajira vijijini, serikali iliongeza juhudi katika sekta ya kilimo ambako vyuo vilivyokuittwatangu uhuri na baada yah apo, ambavyo sasa vinaunda vyombo viitwavyo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI).

Hapo wakapatikana mabwana shamba na mabibi shamba waliosambazwa shambani, kuinua kilimo chao kila mahali na kasi ya uzalishaji chakula na malighafi kuongezeka zaidi na upande wa vijana, kubunjwa taasisis za kuhudumia umma zikawa nyingi sana.

Wakati mpango huo wa miaka mitano unafika tamati mwaka 1969, kukawapo mashirika mengi ya umma nchini, kundi kubwa nkla wafanyakazi, kilimo kimepamba moto nchini sasa taifa kilichukua sura 'kukitumia tunachokizalisha."

Serikali ikaamua kuunda sheria inayosimamia wafanyakazi na mashirika ya umma na ndani yake kukaundwa Tume ya Rais ya Kusimamia Mashirika la Umma inayoitwa (SCOPO).

Ndani ya sheria inayosimamiwa na SCOPO ilikuwa na mengi yanayomhusu mfanyakazi, maslahi na cheo chake, hata ikiupa umaarufu msamiati 'Mshahara wa SCOPO."

- ***Inaendelea Ijumaa ijayo.***

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Safari ya Korea na mauzauza yake-III






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

KATIKA sehemu ya pili ya simulizi hii tamu ya safari ya Korea, wiki jana nilimalizia siku tulipofakamia supu ya vifaranga vya kuku tukiwa na dereva wetu wa Kikorea, Paul!

Siku hiyo kabla ya kuingia kwenye mgahawa huo, Paul aliamua kutuzungusha katika Jiji la Seoul, akijua ndiyo siku yetu ya mwisho kuwa naye katika jiji hilo la kuvutia kwa kila hali.

Tulishuhudia jinsi madereva walivyo na nidhamu barabarani, husikii kelele za honi za magari, sitaki kusema za daladala au bodaboda kwa sababu 'madudu' hayo hayapo huko, bali kuna mabasi ya mwendo kasi kama hapa.

Lakini mabasi hayo hayana barabara maalumu kama hapa, yaani zilizotengwa kwa kuta, bali yanapita sehemu moja na magari mengine hususan madogo, lakini yenyewe ikiwa ni pamoja na malori, yanakuwa na upande, kwenye mstari mmoja.

Maana yake ni kwamba yakikaa kushoto, basi madogo yatakaa kulia na kinyume chake na kumbuka barabara si za kitoto, yaani nyingi ni kama barabara ya kuanzia Kimara hadi Kibaha kwa hapa Bongo, yaani njia nne hadi sita.

Paul anatuambia ukisikia honi basi ujue kuna dharura kubwa na si hapa kwetu, dereva shabiki wa Yanga au Simba, akisikia timu yake imeshinda atapiga honi kuanzia Kibaha mpaka anaingia katikati ya Dar es Salaam.

Bodaboda ndiyo kwanza atafunga honi ya lori kwenye pikipiki yake, akikupigia kwa nyuma, utadhani unavamiwa na Scania kumbe wapi!

Mambo ya vimulimuli ndio usiseme sasa Bongo watu wanafanya mapambo.

Wanashindwa kuachia magari ya dharura kama ya hospitali, polisi na benki, lakini ndio kwanza wanafunga kwenye magari yao, walinzi wa usalama barabarani hata wakionya hakuna linalofanyika, ndio kwanza utaona vimulimuli vinaongezeka barabarani!

Ukienda upande wa ma-Mfugale na ma- Kijazi katika jiji la Seoul, ndio usiseme, huko ni barabara za juu yaani kama kutoka Posta juu kwa juu kupitia Vingunguti mpaka Ubungo na kurudi mjini. Hapa kwetu tunakenulia meno maKijazi na maMfugale eti barabara za juu!

Hilo gari tulilokuwa tukitumia na dereva Paul, thubutu kukuta gia ya kuchomoza kama tendegu la kitanda! Humo ni kubonyeza vitufe kuanzia gia ya kuendesha, kurudi nyuma, kuweka nyuturo na hata kuegesha.

Hakuna kutoa misuli ya mikono na mishipa yake eti unaingiza gia. Upo mlalahoi? Kwa kweli zaidi ya kushangaa maghorofa ya Zumaridi yaliyoko Seoul, tukashangaa aina ya magari yanayotengenezwa hapo, kwa sababu ni ya kisasa zaidi ikilinganishwa na haya ninayoona hapa Bongo!

Kwa kweli magari yanayoingizwa Bongo jamani ni ya kustahili dampo. Tushukuru ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambayo imewezesha kuingia mkataba na kampuni kama ya Hyundai ambayo itakuja kuunganisha magari hapa nchini na kutusaidia kuyapata hapahapa na kwa kiwango.

Na kama Hyundai haitatufanyia shere na kutengeneza kama hayo tuliyoyashangaa Seoul, bila shaka haya ya kutoka Japani tutayatumia kufugia kuku na mifugo mingine, kwa sababu hayatastahili kuingia barabarani.

Lakini, tutayafanya hayo kama tu tutakuwa na miundombinu inayofaa na si kama ilivyo hivi sasa, kwa sababu jambo lingine la kuvutia na kushangaza tuliloona Seoul, ni kwamba nchi ile ya Korea ni ya milima kama ilivyo Mwanza.

Cha kushangaza pia ni kwamba barabara zimepanda milimani na kwingine milima imetobolewa, ili magari na treni ziweze kupita kusafirisha watu na mizigo yao bila kulazimika kuzunguka mlima na kupoteza muda.

Ilinifikirisha jinsi vituo vya treni la kwetu la kisasa vilivyo mbali kutoka makazi ya watu, kiasi kwamba mtu atashuka porini ili kwenda anakoenda au kwao, sijui kwa nini reli ya kisasa haikupita katikati ya miji ili kuleta ushindani na mabasi yenye stendi mijini! Ni mipango tu.

Nikwambieni tena, kwamba Korea suala la hakuna kazi au ajira ni la kusikia kwa mbali tu, kwa sababu kuna miradi mingi ya kilimo cha kisasa lakini pia ujenzi wa majengo mapya tena maghorofa karibu kila mahali.

Ndiyo sababu vijana wa Bongo walioko huko huwaambii kitu. Kama unaambiwa mshahara kwa fedha za madafu kwa mwezi si chini ya milioni mbili unataka nini tena?

Lakini, ole wenu mzamie, hilo halipo huko, utapata ajira kama imeoneshwa hivyo kwenye viza yako, vinginevyo utarudishwa Bongo muda si wake, fuata taratibu huko, ukiheshimu sheria na taratibu, ah mambo mbona muswano.

Mpo? Nilikuwa nahubiri kuhusu nchi ambayo ukubwa wake ni sawa na kuunganisha Tabora na Geita, lakini yenye watu milioni 50 na ushei.

Rais wao huongoza kwa miaka mitano tu, akishamaliza anapelekwa mahakamani kufanyiwa tathmini, kama aliboronga anasogezwa jela na kama alifanya vizuri, anabaki huru. Fikiria sasa, na huku tufanywe hivyo?

BIASHARA

# Wachina wanavyojinusuru kiuchumi kupitia vibubu vya simu za mkononi

**Na Mwandishi Wetu**

"KILA mwaka uishapo tulikuwa na pesa kidogo. Nilihisi kutokuwa salama lakini sikujua la kufanya," anasema Xiao Zhuo, mama wa watoto wawili mwenye umri wa miaka 36, anayeishi jijini Xiamen, Mashariki mwa China.

Wakati wa janga la Uviko 19, Xiao Zhuo na mumewe walilazimika kuchukua mishahara iliyokatwa asilimia 50. Lilikuwa pigo kwao na familia. Alikuwa na mzigo pia wa kumtunza mama yake, aliyegunduliwa na saratani miaka mitano iliyopita.

Imekuwa mtindo kwa vijana wa China, kutafuta washirika - wenye sifa sawa kwenye mtandao. Xiao Zhuo alitafuta watu ambao wana mitazamo ya kuokoa pesa.

A|liiona kwa mara ya kwanza kwenye instagramu, Februari mwaka jana. Imevutia maoni milioni 1.7 tangu wakati huo, kulingana na wachambuzi husika.

Wanachama hao ni wanawake wenye umri kati ya miaka 20 na 40, huku wengi wao kina mama. Wengine wanasema wanataka kuweka akiba kwa ajili ya elimu ya watoto wao, ambayo inazidi kuwagharimu.

Baada ya miaka ya janga la maradhi Covid 19, ufufuaji uchumi wa China ukakabiliwa na gharama ya pango ya majengo, bei ndogo za bidhaa wanazouza, kushuka uwekezaji wa kigeni na kuongezeka deni la serikali mitaani.



Wachina wakiwa katika mijumuiko yao. **PICHA; MTANDAO.**

**HALI YAO ILIVO**

"Huko China, wanawake ndio huwa na jukumu la kugharamia nyumba kila siku. Kuona wanawake wengi wanaweka akiba ni kiashiria kwamba ukosefu wa ajira unaenea - sio tu miongoni mwa vijana," kwa mujibu wa Profesa wa Sera za Umma, Lu Xi, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Singapore.

Kuongezeka haja ya watu binafsi kuweka akiba. kutafanya iwe vigumu zaidi kwa China kusawazisha uchumi wake. Katika miongo kadhaa iliyopita, ukuaji ulichochewa na uwekezaji katika miundombinu na nyumba za bei ya chini.

Kadiri uchumi wa China unavyokua, wataalamu wanasema kuna haja ya kuongeza matumizi ya ndani ili kuendeleza ukuaji.

Xiao Zhuo anakajihisi mwenye bahati, kufanya kazi katika sekta ya nishati safi, sekta inayopanuka ikichangia asilimia 40 ya ukuaji uchumi wa nchi mwaka jana.

Hata hivyo, anasema anajiandakwa magumu, kwani watu wengi katika familia na marafiki zake wanapoteza kazi, wakiwamo anaofanya kazi nao katika huduma za umma, kama vile hospitali na shule.

Mwezi Februari, Xiao Zhuo alijiunga na vikundi vya kuweka pesa. Kila siku, wanachama wanapaswa kuweka bajeti na matumizi yao. Pia wanazuia kufanya matumizi holela.

Xiao Zhuo, anasema kajifunza mbinu za kuweka pesa. Kwa mfano, alijifunza kuhusu programu ya simu inayookoa kila siku sarafu kadha. Baada ya mwaka mmoja, akasema akawa na akiba wastabni Yuan 34,000.

Msukumo wa kufanya ununuzi kwa Xiao Zhuo umepungua. Hapo awali, angeweka chochote alichopenda kwenye toroli kwenye duka kubwa. Lakini sasa, hutengeneza orodha ya mahitaji ya chakula tu aendapo dukani.

Mwezi mmoja baada ya kupata washirika wa kuhifadhi pesa, amepunguza matumizi yake kwa asilimia 40 iwa na matumaini ataokoa yuan 100,000 baada ya mwaka - ongezeko mara kumi kutoka hapo awali.

Wanawake wengine pia wanasema mbinu hiyo imewasaidia kuokoa pesa. Mwanachama mmoja anasema. sasa anajipikia mwenyewe na amepunguza ununuzi usio wa lazima.

Mwingine anasema ameokoa zaidi kwa kujiweka bize kazini na atatafuta mambo mapya ya kumfurahisha ambavyo hayana gharama sana.

**FEDHA NI MFALME**

Baadhi ya wanawake wamechagua njia ya kitamaduni kuhifadhi pesa nyumbani. China ina karibu asilimia watu wanaotumia malipo ya simu,

"Ninahisi salama na kuridhika kuona rundo la noti zikizidi kuwa nene," anasema Mama Chen, mwenye umri miaka 32, anayeendesha biashara ya urembo katika jimbo la kati la Henan.

Kila mwezi, alitoa sehemu kubwa ya mapato yake kutoka benki na kuweka pesa kwenye sanduku. Ikifika Yuan 50,000, ataweka amana ya kudumu.

Sasa, anatumia pesa taslimu kwa ununuzi. Ni usumbufu, anasema, lakini hii ni njia yake ya kupunguza matumizi."

Huku kukiwa na kuzorota kwa uchumi, Chen amepoteza idadi kubwa ya wateja wengi wa kawaida waliopunguza matumizi yao.

Nchini China, wanaume humiliki nyumba wanakapofunga ndoa. Kwa hivyo, ni kawaida kwa wazazi kununua mali kwa watoto wao.

Kwa makadirio yake, familia yake inahitaji angalau yuan milioni tano kama akiba - lakini ana hofu hata hiyo haitatosha kwani sasa ni mjamzito tena.

"Hapo awali, sikuwa na mpango wowote wa kuweka akiba lakini nilikuwa na pesa. Lakini sasa kuwa na pesa mkononi kunanifanya nisiwe na wasiwasi."

• *Kwa mujibu wa BBC*

## EWURA CCC ILIVYOJITWISHA JUKUMU LA SAFARI KUTAFUTA MABADILIKO YALIKO

Inatoka Uk 11

hasa kwa nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania.

Hali hii inasababisha wananchi wengi na baadhi ya taasisi kuendelea kutumia nishati isiyo safi ya kupikia, jambo linaloendelea kuchochea ongezeko la athari za kimazingira, kiafya, kiuchumi na kijamii.

Hata hivyo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza Sera na Mikakati yenye lengo za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.

Pamoja na utekelezaji wa Sera na Mikakati hiyo chini ya Sekta na Taasisi mbalimbali, hakuna mwongozo wa kitaifa unaotoa mwelekeo mahususi wa kuhakikisha jamii yote inatumia nishati safi ya kupikia na kuondokana na nishati isiyo safi.

Kutokana na hali hii, Rais Samia Suluhu Hassan, katika ufunguzi wa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia mwaka 2022 alielekeza kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa utakaotoa mwongozo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwa muktadha huo, serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ambao unatoa mwelekeo wa nchi kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Mkakati huu una lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Baraza linaunga mkono na kutekeleza mkakati huu kwa kauli na vitendo.



# Mbarawa: Safari ya kwanza SGR iko pale pale

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema safari ya kwanza ya treni ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma iliyopagwa kuanza Julai 25, mwaka huu ipo palepale kama ilivyopangwa.

Alitoa ufafanuzi huo juzi baada ya kuhitimisha ziara yake ya kukagua njia ya reli pamoja na miundombinu mingine iliyoanzia Dar es Saalam hadi Dodoma.

Alisema amelizika na maandalizi ya safari hiyo ya kwanza kutokana na kukamilika kwa njia na miundombinu mingine itakayoanza kutumika.

"Ziara yetu tumeianza leo (juzi) asubuhi majira ya saa 12 asubuhi na kufika Morogoro saa moja asubuhi ambapo tuliangalia changamoto zilizopo kwenye safari zilizoanza za Dar es Saalam, Morogoro na baada ya hapo tukaanza safari ya kuja Dodoma kukagua njia na miundombinu mingine," alisema Mbarawa na kuongeza: "Kwa kiasi kikubwa vitu vingi vimekamilika bado changamoto kidogo tuu kama vile kuna eneo bado hawajakamilisha ujenzi wa uzio kwa ajili ya kuzuia tembo kukatiza kwenye reli, lakini wamesema baada ya siku nane itakuwa imekamilika, hivyo kutoa fursa ya kuanza kwa safari hiyo ya kwanza".

Alisema kwa upande wa stesheni zote kuanzia Kilosa mkoani Morogoro hadi Dodoma zimekamilika, hivyo kutoa nafasi kubwa ya kuanza kwa safari hiyo ya kwanza Juali 25, mwaka huu kama ilivyokuwa imepangwa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mhandisi Machibya Shiwa, alisema tayari wamekamilisha mambo yote muhimu yanayohitajika kwa ajili ya kuanza kwa safari hiyo.



Kazi ya kusuka nondo kwa ajili ya ujenzi wa daraja, ikiendelea katika eneo la Kimara Mwisho Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC aagiza kuchukuliwa hatua watakaotajwa na CAG

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameagiza kuchukuliwa hatua kwa wakuu wa idara ambao watazalisha hoja mpya za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kama hatua ya kuimarisha utendaji kazi kwenye halmashauri hizo.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao maalum cha kujadili hoja za CAG cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Dendego alitoa agizo hilo kufuatia Halmashauri ya Manispaa ya Singida kuwa na hoja 64 kutoka mwaka wa fedha 2011 hadi Juni 2024, ambazo hazijafungwa jambo ambalo alisema siyo zuri na linatia dosari katika kutekeleza sheria, kanuni na taratibu za serikali hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alionya kuwa hataki kusikia uzalishaji wa hoja mpya na kama zikitokea basi aliyesababisha hoja hiyo aitwe na kuhojiwa kwa nini hoja hiyo imetokea ikiwezekana achukuliwe hatua. Kadhalika, alisema hoja hizo zinapotokea zinasababishwa na kuwapo kwa kasoro hasa katika usimamizi hafifu wa miradi ya maendeleo.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alikerwa na uwajibikaji hafifu wa watendaji wa Manispaa ya Singida katika kujibu hoja za CAG, licha ya ushauri uliowapatia katika kikao cha kamati ya fedha.

Dk.Mganga alisema mambo mengi walioshauri ambayo yangesaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza hoja za CAG hayajafanyiwa kazi jambo ambalo ameonya lazima likome na watendaji lazima wawajibike ipasavyo katika kuondoa kasoro hizo.

Hivyo, aliwataka wakuu wa idara katika halmashauri za mkoa huo kuacha uzembe na kuhakikisha hawazalishi hoja mpya za CAG na kujibu kwa uhakika hoja zilizopo ili ziweze kufungwa na CAG.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Singida kuwa watafanyia kazi maelekezo yao ili kuhakikisha hoja 64 za CAG zinafanyiwa kazi ili kuhakikisha Manispaa ya Singida inakuwa bora katika utendaji wake wa kazi.

# Wanaotumia nafaka kutengeneza pombe waonywa

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WAKAZI wilayani Bahi mkoani Dodoma wameshauriwa kutumia vizuri mazao yao waliyovuna msimu huu ili kuwa na usalama wa chakula, badala ya kutumia nafaka hizo kwa ajili ya kutengeneza pombe za kienyeji.

Mkurugenzi wa shirika la kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi mkoani hapa (KISEDET), Underson Mdunu, alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Nghulugano wilayani hapa, kuhusu kutumia mazao yao kwa maslahi ya kujiinua kiuchumi badala ya kuelekeza kwenye matumizi ya kupikia pombe.

Mkurugenzi huyo aliwataka wakazi hao kujiwekea akiba ya kutosha ya chakula, ili kukabiliana na baa la njaa ikiwamo kuepuka walanguzi wanaonunua mazao kwa bei ya chini mashambani.

Aidha, aliwataka wakazi hao kutumia mazao mbalimbali waliyovuna kuwekeza kwenye shughuli za uzalishaji na kujiwekea akiba ya kutosha, badala ya kupikia pombe ambayo mara nyingi imekuwa ikileta njaa katika familia.

Kadhalika alitoa wito kwa watu wenye ulemavu, vijana na wanawake kujiandikisha katika daftari la wapigakura na wenye sifa wajitokeze kugombea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika mwaka huu.

Alisema mwaka 2024 utafanyika uchaguzi huo hivyo ni wakati wao kwa makundi hayo kutoogopa kujitokeza kugombea kwenye nafasi hizo kwa watakaona wana sifa za kuwa viongozi.

Mchungaji wa Kanisa la Pentecostal Evangelistie Fellowship of Africa Nghulugano Wilaya ya Bahi, Benjamin Lusinde, aliwataka vijana kujituma kufanya kazi ili kuondokana na ukosefu wa kipato.

Alisema pamoja na kazi ya kumtumikia Mungu lakini wanatakiwa kujishughulisha na fursa zilizopo kwenye maeneo yao zikiwamo kilimo, ufugaji, uvuvi na kilimo cha bustani ili wajiimarishe kwenye vipato vyao.

# Dodoma kinara utoaji habari kwa wananchi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umekuwa wa nne kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa utoaji wa habari kwa wananchi. Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Kaspar Mmuya, alisema hayo jana baada ya kukabidhiwa kikombe na cheti kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kilichopatikana kutokana na umahiri katika utoaji habari kwa vitengo vya mawasiliano serikalini.

Mmuya alisema Mkoa wa Dodoma umeshika nafasi ya nne kati ya mikoa 26 ya Tanzania bara, kutokana na tathmini iliyofanywa na Idara ya Habari Maelezo chini ya wizara katika utoaji taarifa kwa wananchi.

Alisema pamoja na mkoa huo kushika nafasi hiyo ya nne pia kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imeshika nafasi ya 13 na Mji wa Kondoa nafasi ya 15.

Alisema kuwa Mkoa wa Dodoma kutokana na matokeo hayo inaonyesha ni jinsi gani ilivyojipambanua katika kukuza uhuru wa habari ili wananchi waweze kupata taarifa sahihi.

Ofisa Utumishi Mkuu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Lucy Timba, alisema Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na halmashauri zake mbili wamefanya vizuri katika tuzo za umahili wa vitengo vya mawasiliano serikalini kwa utoaji wa habari kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Hellen Minja, alisema kuwa wamejipanga kupiga hatua zaidi.

Tuzo ya umahili wa vitengo vya mawasiliano serikalini vilivyofanya vizuri kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilitangazwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali mbele ya Rais, Juni 18, 2024 katika Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari nchini.





# Serikali: Wakulima yajayo yanafurahisha, tunzeni mazao

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI imewashauri wakulima mkoani Mbeya kutouza mazao ya chakula kwa bei ya chini kwa maelezo kuwa imewaandalia mazingira mazuri ya kuuza mazao hayo nje kwa bei yenye tija zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alitoa wito huo juzi alipokuwa anafunga maonyesho ya kilimo biashara yaliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya.

Maonyesho hayo yaliandaliwa kwa lengo la kuwafundisha wakulima mbinu na teknolojia za kisasa za uzalishaji wa mazao ili kuongeza tija na kuwainua wakulima kiuchumi.

Alisema serikali ina utaratibu wa kuwaandaliwa vibali maalumu wafanyabiashara vya kusafirisha mazao na kwenda kuuza nje ya nchi na hivyo akawataka wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema nchi za jirani hasa za Malawi na Zambia zinakabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango na hivyo akasisitiza kwamba soko hilo litakuwa la uhakika.

"Tunzeni mazao yenu msiwauzie madalali na vishoka maana wanawaharibia soko la mazao yenu, subirini soko likiwa zuri ndipo muuze maana serikali imeandaa mazingira mazuri," alisema Malisa.

Alisema wakulima wengi wanaamini kwamba mwaka huu wamepata mazao mengi lakini wasipokuwa makini wanaweza kuuza mazao hayo yote na kubaki bila chakula.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kituo hicho, Leonard Sabula, alisema waliandaa maonyesho hayo kwa lengo la kuwabadilisha wakulima ili wazalishe mazao mbalimbali kwa tija. Sabula alisema wamekuwa wakiandaa maonyesho hayo kila mwaka na kwamba mbali na maonyesho hayo pia teknolojia hizo zimekuwa zikifundishwa kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane).



Baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wakichoma taka walipokwenda kufanya usafi na kutoa misaada kwa wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka cha jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TARI yabuni mbegu za kisasa kufufua zao la ulezi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimezalisha aina tisa za mbegu za ulezi ambazo inakusudia kuzisajili na kuzisambaza kwa wakulima wa maeneo mbalimbali nchini, ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Mbegu hizo zimefanyiwa utafiti katika mikoa mbalimbali ikiwamo Singida, Rukwa, Katavi, Songwe na Mbeya ambapo inadaiwa wakulima wanashirikishwa kuchagua aina ambazo wanaona zinafaa kabla ya kupelekwa katika Taasisi za Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI).

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Denis Tippe alisema waliamua kuzifanyia utafiti mbegu hizo kwa lengo la kufufua zao hilo ambalo kwa miaka ya karibuni lilikuwa limeanza kupotea kutokana na wakulima wengi kutozalisha.

Alisema walikusanya vinasaba vya aina mbalimbali za ulezi kutoka katika maeneo mbalimbali yakiwamo baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki na kwamba utafiti huo ulifadhiliwa na Serikali ya Norway.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa mazao ya asili ambayo yana umuhimu mkubwa kiuchumi na kiafya na hivyo akawataka wakulima kuchangamkia kilimo cha zao hilo ili kujiinua kiuchumi.

"Ulezi ni muhimu sana kwenye afya za binadamu hasa watoto na wazee, hii ni kwa sababu zao hili lina madini mengi ya zinki na chuma ambayo ni muhimu sana ndio maana uji wa ulezi huwa unauzwa sana mitaani na wengi wanaupenda," alisema Dk. Tippe.

Alisema kutokana na umuhimu wa zao hilo hata soko lake ni kubwa na hivyo akawataka wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia kilimo hicho ili wajiinuwe kiuchumi.

Aliishukuru serikali kwa kuwasaidia kutekeleza utafiti huo akidai kuwa utafiti huo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi, taifa na hata afya za wananchi.

Baadhi ya wakulima wa ulezi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, walisema zao hilo ni muhimu kwao kutokana na kwamba haliozi wala kushambuliwa na wadudu kama ilivyo kwa magonjwa mengine ya nafaka.

Mmoja wa wakulima hao, Elisha Sheyo kutoka wilayani Ileje alisema uzalishaji wa ulezi ni tofauti na mazao mengine kwa maelezo kuwa halina gharama kubwa kama ilivyo kwa mazao mengine.

Alisema zao hilo linavumilia ukame na hali yoyote ya hewa na hivyo wanazalisha bila kutumia nguvu na gharama kubwa kama ilivyo kwa mazao mengine.

Naye Mawazo Nzowa alisema awali walikuwa wanalima zao hilo kwa kiasi kidogo na kwamba walikuwa wanazalisha zaidi kwa ajili ya kutengenezea pombe lakini kupitia elimu waliyopewa na watafiti wa TARI wamebaini kuwa unatumika kwa shughuli zingine.

Alisema kwa sasa wamebaini kuwa zao hilo linaweza likazalishwa kibiashara na likawainua kiuchumi na hivyo akasema utakapofika muda wa kuchangia aina ya mbegu wanazotaka zikasajiliwe watashiriki.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima wa Ulezi, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliwataka wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutembelea vituo vya utafiti ili kujifunza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Aliwataka pia kuwatumia maofisa ugani walioko kwenye maeneo yao ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao hayo na kukuza uchumi wao.

# Bil.14/- zaelekezwa afya, nishati, elimu Makambako

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya Sh. bilioni 14.1 zimetekeleza miradi ya maendeleo katika Jimbo la Makambako mkoani Njombe kwa kipindi cha miaka mitatu, huku mbunge wa jimbo hilo, Deo Sanga akichangia zaidi ya Sh. milioni 490.

Fedha hizo zimetekeleza miradi katika sekta za afya, maji, nishati na elimu katika kipindi cha kuanzia 2021/2022 hadi 2023/2024, kwamba Sh. bilioni 11 zimetokana na serikali kuu, Sh. bilioni 2.1 mapato ya ndani ya halmashauri na wadau mbalimbali wakiwamo wananchi, madiwani na mbunge ikiwa ni Sh. bilioni 1.2.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Keneth Haule katika mkutano wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka mitatu ambayo imewasilishwa mjini humo.

"Kwa upande wa afya naomba kuwakumbusha kwenye hospitali yetu ya Makambako tuna huduma ya mama wajawazito, tuna huduma ya kujifungua na upasuaji zipo pale ambazo zilikuwa zinapatikana maeneo mingine, lakini pia huduma za kulaza wagonjwa wanaume na wanawake zipo pale," alisema Haule.

Haule alisema halmashauri itaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa soko kuu na stendi.

Naye Mbunge wa Makambako, Deo Sanga alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara ambayo imeharibiwa kutokana na mvua zilizonyesha.

Sanga aliwataka watalaamu wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanasimamia kwa uadilifu fedha zinazotolewa na serikali ili ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Awali, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini TARURA Wilaya ya Njombe, Sikiti Pella, alisema wakala huo umejipanga kufanyia kazi changamoto za barabara katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani hapa.

Mtaka pia alitoa rai kwa wanachama wa CCM jimboni humo kuacha tabia ya kukaa na vitu kifuani muda mrefu hali ambayo inasababisha chuki zisizoisha baina yao.



# CCM: Mazrui ukifukuzwa ACT-Wazalendo njoo kwetu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, amesema chama hicho kipo tayari kumpokea Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, endapo atafukuzwa uanachama katika chama chake.

Alitoa kauli hiyo jana baada ya kuwepo kwa tetesi za maandalizi ya kufukuzwa kwa kiongozi huyo kwa madai ya kutoridhishwa na kauli yake aliyotoa hivi karibuni ya kumpongeza Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Mwinyi kwa kazi kubwa ya kuimarisha sekta ya afya Zanzibar.

Mazrui alitoa pongezi hizo wakati wa uzinduzi wa nyumba za wafanyakazi wa Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoa wa Kusini Pemba.

Katibu huyo alisema amepokea taarifa kutoka katika chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya ACT-Wazalendo, kuwa jana baadhi ya viongozi wa Kamati Kuu ya Chama hicho wamekaa kikao cha siri kujadili kwa kina tuhuma zinazomkabili Naibu Katibu Mkuu huyo Nassor Mzrui na idadi kubwa ya wajumbe hao walipendekeza afukuzwe kwani kauli zake zinaipigia kampeni CCM na kuwatosa kisiasa ACT-Wazalendo.

Mbeto, alisema CCM ni mwalimu na kinara wa demokrasia nchini, hivyo kipo tayari muda wowote kuwapokea viongozi mbalimbali wa vyama vya upinzani wanaokiri kwa vitendo na kuunga mkono kazi nzuri ya kuwaletea maendeleo wananchi bila ubaguzi wa kisiasa.

Katika maelezo yake Mbeto, alisema kitendo cha kiongozi huyo Nassor Mazrui kutamka hadharani kuwa kura ni siri hivyo wananchi wana uhuru wa kuchagua chama kinacholeta maendeleo mbele ya Rais wa Zanzibar Dk.Mwinyi imekuwa ni pigo na majanga kwa ACT-Wazalendo kutokana na sera zao za kubeza, kupotosha na kukosoa na kutengeneza propaganda chafu ndidi ya CCM na serikali.

"CCM ni kimbilio la wanasiasa na wananchi wote jambo la msingi ni kuheshimu na kufuata itikadi na sera zetu kwa kutanguliza mbele dhana ya ukweli na uzalendo uliotukuka," alisema na kuongeza:

"Niwaambie wananchi kuwa muda wowote tupo tayari kumpokea kwa mikono miwili Waziri wa Afya na Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo Nassor Mazrui, atakapofukuzwa rasmi na chama chake kwani sababu ya kufukuzwa kwetu tunamuona ni shujaa wa kisiasa na mwenye misimamo isiyoyumba".

Alieleza kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kila mwananchi yupo huru kutoa maoni, hivyo hata ndani ya vyama vya siasa kila kiongozi ana haki ya kutoa maoni yake binafsi na bila kuathiri misimamo ya chama chake.

Hivyo, alitoa wito kwa viongozi wengine ndani ya ACT-Wazalendo waendelee kujitokeza hadharani kuunga mkono msimamo wa Nassor Mazrui, kwani hiyo ndiyo njia pekee ya kujitoa katika jela na utumwa wa kidemokrasia ndani ya chama hicho.

Alisema wakati umefika wa vyama vya upinzani nchini kuachana na siasa za ulaghai na propaganda chafu za upotoshaji badala yake wabadilike na kujenga utamaduni wa kukosoa kwa heshima na kutoa maoni ya kutatua changamoto za wananchi.

Mbeto, alisema mapinduzi ya kisiasa ndani ya vyama vya upinzani yataletwa na viongozi wachache wenye dhamira na misimamo imara na kujitolea katika kulinda maslahi ya wananchi wengi, badala ya kundi la viongozi wachache wanaofanya uwakala na udalali wa kisiasa kwa maslahi ya baadhi ya nchi za kigeni.

Sambamba na hayo alisema CCM itaendelea kuheshimu misingi ya kidemokrasia pamoja na kusimamia kwa vitendo sera zake ziendelee kuwa na manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

# Serikali kufanya ukaguzi maeneo ya watalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale kupitia Kamisheni ya Utalii Zanzibar inatarajia kufanya usajili na ukaguzi wa maeneo ya watalii, ili kuhakikisha ubora na usalama wa huduma hizo zinatolewa katika makazi hayo. Waziri wa wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika kikao cha wadau wa sekta ya utalii kilichofanyika Mjini Zanzibar ambapo alisema mchakato huo utafanyika kwa awamu.

Alisema kwa kuanzia mchakato huo utaanza katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ikihusisha mitaa ya Mji Mkongwe, Mlandege, Michenzani, Chukwani, Mbweni, Fumba, Kama, Chuini na Bububu.

Waziri Soraga, alisema kamisheni itaanza ukaguzi wa makazi hayo kwa ajili ya kuhakikisha kama itakuwa na viwango vya biashara hiyo ya kulaza wageni.

Aidha, alisema licha ya kupatiwa leseni hiyo, pia Kamisheni ya Utalii kwa muda wowote ina uwezo wa kusitisha leseni hizo ikiwa imegundulika kutumia taarifa za ulaghai, upotoshaji au uongo wakati wa maombi hayo.

Alisema: "Kamisheni ya Utalii inaendelea kusisitiza kuwa mtu yoyote ambaye atakiuka masharti yoyote ya kanuni hizo adhabu maalum iliyotolewa na ikithibitika ametenda kosa kubainika anatiwa hatiani na kutakiwa kulipa faini isiyopungua Dola za Marekani 1,000 na isiyozidi Dola za Marekani 5,000.

Naye Katibu wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba, alisema kikao hicho kimekuwa na wadau hao ili kuwakutanisha wadau wa sekta ya utalii na kuweza kupokea maoni katika taasisi zao.

Aidha, alisema pia kamisheni imeandaa maonesho ya utalii yanayotarajiwa kuanza hivi karibuni ambapo alia lengo la kuanzisha maonesho hayo ni kuona sekta ya utalii inakuwa nchini.

Hivyo, aliwaomba wadau hao kuendelea kuwaunga mkono ili kuona wanafanikisha maonesho hayo kwani asilimia kubwa ya mapato ya Zanzibar yanatoka katika sekta ya utalii.




Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Laurence Mafuru (katikati), akizungumza wakati wa mkutano wa kujadili mipango ya maendeleo na nini kifanyike kuelekea kufikia mwisho wa ukusanyaji maoni na uandishi wa Dira 2050, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkandarasi Bandari ya Shumba akalia kuti kavu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (WUMU), Dk. Mngereza Mzee Miraji, amesema wizara yake haijaridhishwa na kasi ya maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini.

Bandari hiyo inayojengwa na kampuni ya COMFIX, aliitaka kampuni hiyo kuongeza kasi ya ujenzi ili kukamilika kwa wakati.

Dk. Mngereza alisema hayo wakati akizungumza na uongozi wa kampuni hiyo uliofika katika ofisi za wizara hiyo kwa ajili ya kujadili changamoto zinazosababisha kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huo.

Katika majadiliano hayo, Dk. Mngereza aliuagiza uongozi wa kampuni hiyo kuzingatia masharti yaliyomo kwenye mkataba baina yao, sambamba na kuzingatia ubora wa kazi wakati wa utekelezaji wa mradi huo, alioutaja kuwa ni muhimu kwa jamii na uchumi wa nchi.

Alisema kuwa serikali imeamua kujenga bandari hiyo ili kurahisisha mawasiliano baina ya eneo hilo na maeneo mengine, lakini pia kuimarisha usalama.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wake kutairasimisha, hivyo kupunguza vitendo vya ukiukwaji wa sheria vikiwamo vya uingiaji.

Mkurugenzi wa Kampuni ya COMFIX, Hashim Lema, alisema kwamba kampuni itarekebisha changamoto zilizojitokeza ambapo aliahidi ndani ya kipindi cha Julai mwaka huu hatua ya ujenzi wa geti itakamilika kwa hatua uwekaji wa vizuwizi (block) na uwekaji wa mawe.

Bandari hiyo ni miongoni mwa bandari zilizoahidiwa kujengwa na serikali kwa lengo la kuimarisha sekta ya usafirishaji baharini.

## HALI YA SEKTA YA HABARI

# Utafiti waibua mambo yanayoshtua

**Na Jenifer Gilla**

UTAFITI uliofanywa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), umebaini wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vya uandishi wa habari nchini hawapikwi ipasavyo, hivyo wanapendekeza mikakati ya pamoja kuondoa kadhia hiyo.

Matokeo ya utafiti huo yaliyowasilishwa jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Hali ya Sekta ya Habari Tanzania kwa Mwaka 2022-2023, yamekuja na mapendekezo matano ambayo yanahitaji ushiriki wa wadau wote kuyatekeleza.

Utafiti huo ulilenga kuhakikisha vyombo vya habari vinatekeleza majukumu yake kwa weledi na utashi na kupongeza pale ambapo vimefanya vizuri.

Akiwasilisha matokeo ya utafiti huo, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini, Tawi la Dar es Salaam (TUDARCo) , Dk. Samwilu Mwaffisi, alisema waligundua wahitimu wanakosa stadi za uandishi kwa sababu hawapikwi vizuri vyuoni.

Dk. Mwaffisi ambaye ni kiongozi wa watafiti hao, alisema waligundua kuwa wanafunzi hao hawapikwi vizuri kwa sababu mbalimbali, ikiwamo mafunzo kwa vitendo kutolewa kwa kiwango kidogo kutokana na uhaba wa vifaa vya kufundishia.

Alisema waligundua pia kuwa vyuo hivyo vinazidiwa na wingi wa wanafunzi, hivyo kushindwa kuwapa mafunzo ya vitendo kwa kiasi kinachotakiwa kutokana na uhaba wa vitendea kazi.

Mtafiti huyo pia alisema wamegundua walimu wanaofundisha wanafunzi hao hawana uzoefu wa kufanya kazi katika vyombo vya habari, hivyo kujikita zaidi katika nadharia.

Alisema hali hiyo inatokana na mfumo uliowekwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) unaoelekeza walimu wanaofundisha vyuoni wawe na shahada ya kwanza yenye ufaulu wa GPA isiyopungua 4.0, kigezo ambacho wengi wenye uzoefu wanashindwa kufikia.

Alisema pia waligundua baadhi ya wanafunzi hawana utashi wa kujifunza kwa sababu wengi wao hawakupenda kozi husika, bali walilazimika kwa kuwa hawakuwa na namna nyingine.

"Wanaokwenda chuo kikuu wanakuwa wana changamoto ya kuelewa lugha ya Kiingereza, hivyo hawaelewi vizuri wanapofundishwa, hawawezi kujieleza hata kuuliza maswali," alisema.

Alisema ni wakati mwafaka kwa TCU kuruhusu waandishi wa habari wenye uzoefu katika vyombo vya habari kufundisha vyuo vikuu ili kupata wanafunzi walioiva.

Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Mary Kafyome, alisema kuwa wakati wanafanya utafiti huo, waligundua kuwa vyombo vya habari hivi sasa vinapitia changamoto kubwa kiuchumi.

Alisema wakati anahoji wahusika wa vyombo vya habari vya serikali, walithibitisha kuwa kama serikali isingekuwa inatoa ruzuku ya mishahara, hali yao ingekuwa mbaya.

Alisema zamani vyombo vya habari vya binafsi vilikuwa vinafanya mbinu mbalimbali kukabiliana na anguko la kiuchumi kama vile kuandaa matamasha, lakini hivi sasa inashindikana kutokana na shughuli hiyo kufanywa na wasanii.

Alisema anguko la kiuchumi linasababisha kukosekana mafunzo ya ndani kwa waandishi wachanga, hali inayosababisha kutotekeleza majukumu yao kwa weledi na kutoa kazi zisizo na ubora unaotakiwa.

"Hata fedha za kufanya uandishi wa kiuchunguzi na fedha za kuongeza vifaa vipya vya kisasa zinakosekana. Utendaji kazi hafifu wa waandishi wa habari wanaochipukia unasababishwa na uchumi mbovu unaoandama vyombo vya habari," alisema.

Mary pia alisema aligundua kuwa ujumuishi wa makundi mbalimbali katika maudhui umeendelea kuimarika kulinganisha na miaka 10 iliyopita, jambo lililochangiwa na kampeni ya mitandao inayotetea haki za watu hao kama vile wanawake, wenye ulemavu na watoto na kuwapo waandishi wa habari wanawake katika nafasi za juu za uongozi.

Mwandishi wa Habari Mkongwe, Hawra Shamte alisema kuwa kwa upande wa Zanzibar, aligundua kuwa waandishi wa habari hawafanyi kazi vizuri kutokana na kubanwa na vipengele vilivyomo katika sera na sheria zinazowasimamia.

Alisema aligundua pia waandishi wanadhibitiwa na wamiliki wasiandike habari zinazoongelea vibaya serikali kwa kuwa wanataka kujenga urafiki na serikali na si kuwa maadui.




Shamte alisema suala hilo limesababisha habari za uchunguzi kupungua kwa kuwa utoaji taarifa unapungua na pia baadhi ya taarifa za serikali zikitolewa, waandishi wanaingia matatani.

Alisema wakati anafanya utafiti, alizungumza na wasomaji habari na wengi wao walisema hawaridhishwi na namna waandishi wa habari wanavyotekeleza majukumu yao, wengi wakionesha dalili za kukosa mwamko.

Alisema pia aligundua waandishi wa habari wengi wanaripoti matukio ambayo yanawaingizia kipato, na wakitwa kwenye kazi ambazo hazina malipo, ushiriki wao unakuwa mdogo.

Alisema hao pia wapo duni katika utambuzi wa mambo, hali inayotokana na kukosa mafunzo ya kina ya namna ya kuandika habari hizo, na kutopata mwongozo wa kutosha kutoka kwa wahariri wao.

"Sisi wakati tunaandika, mwandishi alikuwa anaipenda kazi yake, tulikuwa tunafundishwa kusoma habari yako ikishatoka ili kujua makosa yako," alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT), Emmanuel Bulendu, alisema licha ya serikali kuboresha vifungu vya sheria vilivyokuwa vinaminya uhuru wa waandishi, bado kuna ambavyo havijafanyiwa kazi na vimebaki kuwa mwiba kwa tasnia.

Alisema kuwa licha ya kukua kwa kasi kwa teknolojia, vyombo vya habari nchini vipo nyuma katika utekelezaji wake hasa suala la akili mnemba.

Alisema licha ya uhitaji mkubwa wa teknolojia hiyo, vyuo vya habari nchini kote havijaanza kutoa mafunzo ya akili mnemba na hakuna sera wala sheria na miongozo ambayo inasaidia waandishi wa habari kuitumia.

Mgeni Rasmi katika hafla hiyo, Waziri Mkuu, mstaafu Jaji Joseph Warioba, alikumbusha waandishi wa habari kuzingatia wajibu wa taaluma yao ya kutoa habari za uhakika zisizoegemea upande mmoja.

Jaji mstaafu Warioba alisema kuwapo sera za vyumba vya habari hakupaswi kuwafanya kusahau jamii inayotegemea kupata taarifa kutoka kwao na kuandika habari zenye mrengo wa propaganda.

Alisema kuna baadhi ya vyombo vya habari vilivyoshirikiana na vyombo vya habari vya nje, vinatumika kutoa habari zinazonufaisha mataifa hayo na kusahau wajibu wao kwa taifa.

Alisema pia uoga uliojengeka kwa waandishi wa habari, wananchi na viongozi unachangia kutoandikwa habari za uhakika kwa kuwa kila mmoja anahofia kuweka maisha yake hatarini.

Alitoa mfano kuwa mwananchi anaweza kuwa na habari, akaogopa kumweleza mwandishi kwa kuhofia usalama wake, viongozi nao wamekuwa wakisifia tu serikali pasi na kuikosoa.

"Katika nchi hii kiongozi yeyote anayesimama hazungumzi sentensi mbili bila kumsifia Rais, lakini ukija mambo mengine anasita," alisema.

Katibu Mkuu mstaafu wa MCT, Kajubi Mukajanga alisema ili kubabiliana na changamoto hizo baraza linapendekeza vyama vya kihabari vifanye mazungumzo na TCU na vyuo vya uandishi wa habari, ili kupata suluhisho la kudumu kwa wahitimu hao ambao wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi na kukidhi mahitaji ya soko.

Alisema baraza limependekeza wadau wa vyombo vya habari na wanaharakati wengine wanapaswa kuongeza juhudi za kutetea mapitio na marekebisho ya sheria zilizopo na kutunga sheria zinazowiana na vyombo vya habari.

Mukajanga pia alisema baraza limependekeza serikali zote mbili kupitia na kurekebisha sheria zilizopo ili kuweka mazingira mazuri zaidi kwa waandishi wa habari kufanya kazi kitaalamu.

Alisema baraza pia limependekeza suala la sera la jinsia katika vyumba vya habari kuwa na lazima na linapaswa kuwa ni mojawapo ya masharti ya kupata leseni.

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**HAWA ISMAIL MAGESA** angantaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya Boxer yenye usajili namba **MC 703 DMK.** Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/KIN/133540/2024**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**FURAHA IBRAHIM DAUD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1756/0009/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **CENTRAL BUHONGWA SEC.SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/134072/2024**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**ELICE HAULE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0219/0065** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **SONGEA GIRLS SEC.SCHOOL** mwaka 2007 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0221/0531** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia WERUWERU SEC SCHOOL mwaka 2010. Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/MUF/9575/2024, PHQ/IRI/MUF/9581/2024.**

**NOTICE YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Madalali tajwa hapo chini kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa wadaiwa kulipa madeni yao. Baada ya hapo hatua nyingine za kishereria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mikopo kama ilivyotangazwa gazetini,

| Mdaiwa/Mdhamini | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| BIN SAAD LTD | Gari T. 928 DMU, Scania R-520 - Dalali Yard | 19/07/2024 | RAPITECH Solutions Ltd |
| William Patrick Chiboni/ Getrude Achard Njau | Gari T.656 DPD Land Cruiser Prado -Tabata yard | 19/07/2024 | KING Africa General Enterprises |
| Daphroser Abeid Hamza /HP Planners & Event Management | Nyumba/Kiwanja – Kata ya Somangila Kigamboni | 26/07/2024 | KING Africa General Enterprises |
| Omary Said Magoma/ Mwajuma Magori | Nyumba- Mbagala Kiburugwa | 30/07/2024 | KING Africa General Enterprises |
| Ramadhan Omary Kerengénye/Donath Mallya | 'Nyumba- Mtaa Kwa Mzungu - Mbagala | 30/07/2024 | KING Africa General Enterprises |
| Pili Shabani Salum | Nyumba - Makurumula Kinondoni | 26/07/2024 | KING Africa General Enterprises |

**Masharti Mengine:**

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**KING AFRICA: 0687956756/0718399636**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**RAPITECH Solutions Ltd: 0755264606**

# Biden akataa kujiuzulu

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAKATI shinikizo la kumtaka kujiondoa kama mgombea wa Chama cha Democrat, Rais wa Marekani Joe Biden, amesisitiza kuwa hatafanya hivyo kamwe.

Kiongozi huo anafanya kazi ya kuwatuliza wanachama wa Democratic baada ya kushindwa katika mdahalo wake wa kwanza na mpinzani wake Donald Trump, wiki iliyopita.

Taarifa za awali zilisema kwamba Biden alikuwa akitafakari mustakabali baada ya tukio hilo.

Jana Rais Biden alikula chakula cha mchana kwa faragha na Makamu wake, Kamala Harris katika Ikulu ya White House na kuongeza uvumi kuwa alikuwa akimshawishi kuchukua nafasi yake kama mgombeaji wa chama katika uchaguzi utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Hata hivyo, viongozi hao baadaye walijiunga na kampeni ya chama chao na hapo Rais Biden aliweka wazi kuwa ataendelea kwenye kinyang'anyiro hicho na Harris alimuunga mkono.

„Mimi ndiye mteule wa Chama cha Democratic. Hakuna mtu wa kuniondoa. Siondoki," alisema Biden kulingana na BBC News.

Maneno hayo hayo yalirudiwa katika barua pepe ya kuchangisha pesa za kampeni iliyotumwa saa chache baadaye.

„Wacha niseme haya kwa uwazi na kwa urahisi niwezavyo, ninagombea," alisema Biden katika barua pepe hiyo, na kuongeza kuwa atakuwa kwenye kinyang'anyiro hicho hadi mwisho.

Maswali yamekuwa yakiibuka iwapo kiongozi huyo mzee mwenye umri wa miaka 81, ataendelea na kampeni yake kufuatia mdahalo huo na Trump, ambao alikuwa na ubabaikaji, sauti dhaifu na baadhi ya majibu ambayo yalikuwa magumu kusikika.

Hali hiyo ilizusha wasiwasi ndani ya chama cha Democratic kuhusu uwezo wake na kushinda uchaguzi huo.

Shinikizo la kumtaka Biden kujiuzulu limeongezeka siku chache tu kwa sababu kura nyingi zinaonyesha kuwa mpinzani wake wa chama cha Republican anazidi kupata umaarufu.

Kura ya maoni ya New York Times, iliyofanywa baada ya mjadala huo, ambayo ilichapishwa Jumatano, ilionyesha kuwa Trump alikuwa akishikilia uongozi kwa mbali zaidi akiwa na alama sita.

Kura nyingine ya maoni iliyochapishwa na mshirika wa BBC wa Marekani CBS News ilionyesha kuwa Trump ana pointi tatu mbele ya Biden katika majimbo muhimu. Kura hiyo pia ilionyesha kuwa rais huyo wa zamani alikuwa anaongoza kitaifa. ***BBC***




Kiongozi wa Chama cha Labour nchini Uingereza, Keir Starmer, akijibu swali baada ya kufanya kampeni katika uwanja wa michezo wa Caledonian Gladiators katika eneo la East Kilbride, Scotland juzi. **PICHA: AP**

# Chama kipi kitaibuka na ushindi Uingereza

**LONDON,** UINGEREZA

RAIA wa Uingereza jana walijitokeza katika vituo vya upigaji kura kuwachagua wabunge katika uchaguzi mkuu wa kwanza uliofanyika Julai tangu 1945.

Watu walipiga kura katika vituo mbalimbali vya kupigia kura, vilivyowekwa katika majengo ya umma kama vile shule za mitaa, makanisa na kumbi za jumuiya.

Upigaji kura ulianza majira ya saa 1:00 asubuhi.

Takriban wapigakura milioni 46 wana sifa ya kuwachagua wabunge 650 katika Bunge la Chini.

Matokeo ya kila eneo, yalitarajiwa kuanza kutangazwa usiku na kuendelea leo.

Chama kitakachounda serikali kinatakiwa kushinda zaidi ya nusu ya viti, 326.

Uchaguzi huo, ulioitishwa na Waziri Mkuu Rishi Sunak mwezi Mei, unafanyika chini ya mipaka ya majimbo mapya kufuatia tathmini iliyopangwa ili kuzingatia mabadiliko ya idadi ya watu.

Mipaka hiyo mipya, kulingana na takwimu za usajili wa wapigakura, imeifanya Uingereza kuwa na wabunge 10 zaidi, na kufikisha jumla ya viti vyake hadi 543.

Idadi ya viti nchini Wales imepungua kwa viti vinane hadi 32, huku jumla ya viti vya Scotland ikishuka kutoka 59 hadi 57. Ireland ya Kaskazini imesalia sawa na viti 18.

Mtu yeyote aliye na umri wa miaka 18 au zaidi anaweza kupiga kura, ikiwa amesajiliwa na ni raia wa Uingereza au raia anayehitimu wa Jumuiya ya Madola au Jamhuri ya Ireland.

Kufuatia mabadiliko ya kisheria mwaka wa 2022, takriban raia milioni mbili wa Uingereza ambao wamekuwa wakiishi nje ya nchi kwa zaidi ya miaka 15 walijiandikisha kupiga kura.

Matokeo ya awali yatakayochapishwa muda mfupi baada ya vituo kufungwa saa nne usiku yatatoa taswira ya kwanza ya jinsi uchaguzi ulivyofanyika katika ngazi ya kitaifa.

***BBC***

## Makubaliano yanukia Gaza

**GAZA, Palestina**

KUNDI la Hamas limesema limewasilisha maombi mapya kwa wapatanishi yenye lengo la kumaliza vita na Israel iliyodumu kwa miezi tisa.

Hata hivyo, serikali ya Israel imethibitisha kupokea maombi hayo kutoka kundi la Hamas, ikieleza itatoa jibu lake kwa wapatanishi.

Mapigano makali yanaendelea na kusababisha idadi ya vifo kuongezeka na kuweka mazingira magumu kwa raia wa Ukanda wa Gaza.

Pande zote mbili zinakabiliwa na shinikizo la kimataifa wakitakiwa kufikia mapatano ya kusitisha vita, kwa msingi wa mpango uliopendekezwa na Rais wa Marekani Joe Biden.

Hamas ilisema katika taarifa iliyotolewa Jumatano jioni kuwa kiongozi wake wa kisiasa anayeishi Qatar, Ismail Haniyeh, alifanya mawasiliano na nchi wapatanishi Qatar na Misri kuhusu mawazo ambayo kundi hilo linajadiliana kwa lengo la kufikia makubaliano.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau na idara ya ujasusi ya nchi hiyo, Mossad, zilithibitisha mkakati huo mpya zikieleza nchi hiyo ilikuwa inatathmini msimamo wa Hamas na kwamba itatoa jibu lake kwa wapatanishi.

Gazeti la New York Time, liliripoti kuwa majenerali wakuu wa Israel wanataka kusitishwa vita Ukanda wa Gaza hata kama itaibakisha Hamas madarakani kwa wakati huu.

Kumeongezeka mpasuko kati ya jeshi na Netanyau ambaye amepinga makubaliano yoyote yatakayoiacha Hamas kuendelea kutawala Gaza.

Makamanda hao wa kijeshi wanaamini kusitishwa vita itakuwa njia bora zaidi ya kuachiliwa huru kwa mateka waliosalia na wanafikiri vikosi vya Israel vimechoka na vinakabiliwa na uhaba wa silaha.

Viongozi hao wa kijeshi wanaamini wapiganaji wanahitaji kujipanga upya iwapo vita vitazuka na kundi la Hezbollah la nchini Lebanon.

Wakati huo huo, shambulizi lililofanywa na vikosi vya Israel usiku wa Jumatano, lilimuua kamanda wa juu wa Hezbollah Mohammed Nasser.

Shambulio hilo lilifanyika kusini mwa Lebanon na kusababisha majibu makali kutoka kwa kundi hilo kwa kufyatua msururu wa maroketi kuelekea kusini mwa Israel.

***DW***



Wacheza-ji wa Timu ya Kitunda FC, waki-wania mpira wakati wa ma-zoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Michezo kubahatisha kuchangia uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

UWEPO wa michezo ya kubahatisha nchini kuna changia uchumi wa nchi kutokana na kodi zinazolipwa.

Hayo yamesemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Ithuba Afrika, Charmaine Mabuza, wakati wa kupokea leseni za kuendesha michezo hiyo hapa nchini.

Alisema wadau wa michezo hiyo wanatambua namna wanavyoongeza pato la taifa huku pia wakiendeleza sekta ya michezo hapa nchini.

"Tunayo furaha kubwa kukabidhiwa leseni, na sisi tutakuwa sehemu ya wachangiaji katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia kodi zitakazokuwa zikilipwa," alisema Mabuza.

Alisema hata mwananchi mmoja mmoja anaweza kuinua kipato kupitia michezo hiyo ya kubahatisha na kushukuru mazingira mazuri ya kufanya biashara hapa nchini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Balozi Modest Mero, alisema bodi hiyo ina jukumu ya kufuatili na kusimamia kanuni zote za kuendesha michezo ya kubahatisha nchini.

Aliipongeza Ithuba kwa kupata leseni na kuwataka kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

# COASTAL UNION YATAKA HESHIMA 'KAGAME CUP'

**Na Shufaa Lymo**

SIKU moja baada ya kupangwa makundi ya michuano ya klabu bingwa Afrika Mashariki ,Kagame Cup', uongozi wa klabu ya Coastal Union umesema utayatumia mashindano hayo kurejesha heshima ya klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Klabu hiyo, Omari Ayoub alisema anaamini wachezaji wao watafanya vema kutokana na maandalizi ya muda mrefu waliyoyafanya.

"Kupitia mashindano haya tunataka turudishe heshima yetu ya mwanzo kwa kulibeba kombe hili kutokana na aina ya wachezaji tuliokuwa nao, alisema Ayoub.

Aidha, alisema Kocha wao mkuu, David Oumna aliwasili mapema kuhakikisha anaandaa mapema timu na kutoa mbinu zake kwa wachezaji ili watimize malengo yao.

Aliongeza kuwa wanayapa umuhimu mkubwa mashindano hayo kwa kuwa yatawasaidia kukijenga kikosi chao kuelekea kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tutashiriki Shirikisho Afrika, tumesajili wachezaji wapya kuimarisha kikosi chetu, tunaamini michuano hii ya Kagame itakuwa kipimo kizuri kwetu kabla ya kwenda Shirikisho," alisema Ayoub.

Alisema kuwa hakuna timu yoyote wanayoihofia katika kundi lao na wapo tayari kupambana ilikulibakisha kombe hilo hapa nchini.

# KMC YASAJILI KIUNGO WA KAKAMEGA HOME BOYS

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imefanikiwa kumsajili kiungo mshambuliaji, Oscar Paul kutoka Kakamega Home Boys ya Kenya.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, amesema mchezaji huyo raia wa Tanzania amesajiliwa ili kukiongezea nguvu kikosi hicho kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu.

Kabla ya kutimkia nchini Kenya, Oscar alikuwa akiicheza klabu ya Prisons msimu wa 2022/23, kabla ya kutimkia nchini humo kusaka malisho.

**"Nawatangazia wana Kinondoni na wadau wote mpira nchini kwamba tumekamilisha uhamisho wa nyota wa kimataifa wa Kitanzania ambaye msimu uliopita alicheza Ligi Kuu nchini Kenya katika klabu ya Kakamega Home Boys, Oscar ni mmoja kati ya nyota wapya ambao tumewaongeza kwa lengo la kupigania malengo ya klabu msimu ujao," alisema Chukuchuku.**

Pia klabu hiyo imesajili kinda wa timu za taifa ya Tanzania za vijana chini ya miaka 17 na 20, Nickson Mosha kwa ajili ya kuimarisha eneo lao la ulinzi.

Beki huyo wa kati ni mmoja kati ya wachezaji tegemeo akiwa ameanzia soka lake katika kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar.

Wakati huo huo, klabu hiyo imemwongeza mkataba kocha wake raia wa Somalia, Abdihamid Moallin, ili aendelee kukinoa kikosi hicho kwa mara nyingine tena msimu ujao.

Kocha huyo aliiongoza timu hiyo kumaliza ligi ikishika nafasi ya tano kwa pointi 37, akiwa ametoka klabu ya Azam FC.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA CALAFIORI

ARSENAL imeandaa kuwasilisha tena dau la pauni milioni 47 kwa ajili ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Italia, Riccardo Calafiori, ambayo awali ilikataliwa na Bologna hao. Chelsea pia inatajwa inataka huduma ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### UNITED, BRUNO KITAELEWEKA

MANCHESTER United itakubaliana na uamuzi utakaochukuliwa na kiungo wa Ureno mwenye umri wa miaka 29, Bruno Fernandes, lakini wakiwa na matarajio atakubali kusaini mkataba mpya wa kubakia Old Trafford. ***(Mirror)***

### SALIBA KUONDOKA ARSENAL

BEKI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, William Saliba, mwenye umri wa miaka 23, anajiandaa kuondoka Arsenal katika majira ya joto, huku Real Madrid ikitajwa imevutiwa na mchezaji huyo. ***(Mirror)***

### OSIMHEN KAMBINI NAPOLI

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen anatarajiwa kujumuishwa katika kikosi cha Napoli kitakachoingia kambini kwa ajili ya kufanya maandalizi ya msimu mpya yatakayoanza wiki ijayo huku Manchester United, Chelsea na Arsenal zinatajwa kumhitaji nyota huyo. ***(Football Italia)***

### WEST YAMKOMALIA TODIBO

WEST Ham inajiandaa kuwasilisha ofa mpya ya kumsajili beki wa Nice na Timu ya Taifa ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, Jean-Clair Todibo, baada ya ofa yao ya awali ambayo ilikuwa ni pauni milioni 25 kukataliwa. ***(Mail)***

### BARCA KUMBAKISHA FATI

ANSU Fati ameondolewa kwenye orodha ya wachezaji wa kuhama Barcelona huku klabu hiyo ikiwa na nia ya kumwona mchezaji huyo akirejea katika ubora wake katika msimu ujao wa 2024/2025***(Mail)***.

### ZIRKZEE ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inatazamia kukidhi kipengele cha kuachiliwa kwa Joshua Zirkzee huku wakipanga kumuuza Mason Greenwood ili kufadhili mpango huo, nao Everton wakitakiwa kuwasilisha ombi jingine kwa Jarrad Branthwaite.***(Mail)***

### BRANTHWAITE MAMBO BADO

KLABU ya Everton inatarajia Manchester United itawasilisha ofa nyingine kwa beki wa England, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21. ***(Liverpool Echo)***

### NDIAYE AKARIBIA EVERTON

EVERTON inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Senegal, Iliman Ndiaye, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Marseille ya Ufaransa. ***(Footmercato)***

### JOSELU SAFARI IMEIVA

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Joselu mwenye umri wa miaka 34, anakaribia kuondoka Real Madrid baada ya kupokea ofa kutoka kwa klabu ya Qatar Al Gharafa. ***(Athletic)***

### GUIU KUONDOKA BARCELONA

CHELSEA imeanza mazungumzo na Barcelona kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wa Hispania, Marc Guiu, mwenye umri wa miaka 18. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID KUMTAMBULISHA RASMI MBAPPÉ JULAI 16

●●● Utambulisho wa Mfaransa huyo huenda ukavunja rekodi ya...

**MADRID** HISPANIA

REAL Madrid inatarajiwa kumtambulisha rasmi nyota wake mpya, Kylian Mbappe, mbele ya mashabiki 80,000 kwenye dimba la Santiago Bernabeu ifikapo Julai 16, mwaka huu.

Madrid ilitangaza hadharani juu ya usajili wake mwanzoni mwa Juni na kutangaza Mbappe atajiunga nao baada ya kuondoka Paris Saint-Germain.

Lakini taarifa ya klabu hiyo ilikuwa na maneno 73 pekee.

„Real Madrid CF na Kylian Mbappe wamefikia makubaliano ambapo atakuwa mchezaji wa Real Madrid kwa misimu mitano ijayo," hadi sasa ni uthibitisho pekee kutoka kwa Los Blancos wamemsajili mchezaji bora zaidi wa kizazi chake.

Hiyo itabadilika hivi karibuni kwa sababu ni desturi kwa Madrid kuzindua zulia jekundu kwa wachezaji wakuu wapya, hebu fikiria ujio wa Cristiano Ronaldo mwaka 2009.

Lakini AS imeripoti klabu hiyo inakusudia kuwa „onyesho la kuvutia zaidi kuwahi kutolewa kwa utambulisho Mbappé.

Julai 16, mwaka huu, Mbappe ataripoti katika mji mkuu wa Hispania, tarehe hiyo imepangwa bila kujali kama Ufaransa itafika fainali ya Euro 2024 siku mbili mapema, na hapo awali atapitia taratibu za matibabu yake. Siku hiyo mchezaji huyo ataibuka kutoka chumba cha kubadilishia nguo cha Bernabeu kwenye barabara ya juu iliyoambatana na moto, huku nyota kike wa muziki kutoka Marekani, Taylor Swift, akitarajiwa kutumbuiza.

Wakati muziki ukichezwa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 atafuata barabara ya umbo la L hadi kwenye jukwaa mbele ya Fondo Norte ambapo Rais wa klabu hiyo, Florentino Perez na Rais wa heshima, Pirri watakuwa wakisubiri.

Mbappe atakuwa amevalia jezi kamili za Madrid zenye jina lake na namba yake mpya.

Kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka, atavaa jezi namba tisa, ambayo mara ya mwisho ilitumiwa na Mfaransa mwenzake na nguli wa Madrid, Karim Benzema.

Lakini, kama ilivyokuwa kwa Ronaldo miaka 15 iliyopita, inatarajiwa muda tu hadi jezi yake anayopendelea ipatikane, huku Mbappe akichukua jezi namba 10 inayovaliwa na Luka Modric mwaka ujao.

# MOKWENA ATUPIWA 'VIRAGO' MAMELODI

**JOHANNESBURG,** AFRIKA KUSINI

KLABU ya Mamelodi Sundowns imethibitisha kuachana na kocha wake mkuu, Rhulani Mokwena.

"Sundowns inapenda kutoa shukurani zake kwa Rhulani Mokwena kwa mchango wake katika mafanikio ya klabu katika kipindi chake kama kocha mkuu," imeeleza taarifa hayo.

Taarifa ya Mamelodi imeeleza kocha huyo atakuwa sehemu ya familia ya timu hiyo na klabu inamtakia kila la heri.

"Uamuzi wa Mamelodi Sundowns ulichukuliwa na bodi kwa kuzingatia malengo na matarajio ya klabu na haukushawishiwa au kulingana na mapendekezo ya mtu yeyote anayehusishwa na klabu," imefafanua taarifa hiyo.

Aidha Kocha, Manqoba Mngaithi na timu ya ufundi wataendelea kuongoza na kudhibiti mazoezi na maandalizi ya wachezaji kwa ajili ya msimu ujao, imeeleza sehemu ya taarifa hiyo.



## Foden amwonea huruma Southgate

**BERLIN,** ENGLAND

PHIL Foden amesema wachezaji wa England lazima walaumiwe kwa uchezaji wao wa kutetereka katika michuano ya Euro 2024, akiongeza "anamhurumia" Kocha Mkuu, Gareth Southgate.

Southgate amekuwa akikosolewa vikali na mashabiki na vyombo vya habari kuhusu uteuzi wa timu na mbinu zake katika muda wote wa michuano hiyo huku England walimaliza kileleni katika Kundi C kabla ya kufuzu kwa pambano lao la hatua ya 16 bora dhidi ya Slovakia katika muda wa ziada.

England itamenyana na Uswisi katika mechi ya hatua ya robo fainali itakayochezwa leo, na Foden alisema ni wakati wake na wachezaji wenzake kuongeza kasi.

"Wachezaji wanapaswa kuchukua baadhi ya lawama," alisema Foden.

"Lazima wawepo baadhi ya viongozi ili kujumuika na kutafuta suluhu kwa nini haifanyiki kazi.


"Kuna mengi tu ambayo kocha anaweza kufanya. Anakuweka katika mfumo na kukwambia jinsi ya kucheza. Ikiwa haiendi hivyo, inabidi namna nyingine.

Foden alisema mtindo wa uchezaji wa England hawendani na maelekezo yao ya mazoezi, akisema Southgate amekuwa akiwaambia waongeze kasi uwanjani.

"Namwonea huruma Gareth," aliongeza Foden. Katika mazoezi, amekuwa akitwambia tuwe juu uwanjani na ninahisi kama wakati mwingine, lazima itoke kwa wachezaji.

"Lazima tuwe viongozi. Katika michezo tungeweza kukusanyika zaidi kidogo na kutafuta suluhu.

"Kwa hivyo ndiyo, tumezungumza zaidi kuhusu hilo. Iwapo itatokea tena kwenye mchezo, tunaweza kukusanyika na kutafuta suluhu, tuone pale inapokosea na kurekebisha vyombo vya habari vyetu."



## Barca sasa kumbakiza Fati

**BARCELONA,** HISPANIA

ANSU Fati ameondolewa kwenye orodha ya wachezaji wa kuhama Barcelona huku klabu hiyo ikiwa na nia ya kumwona mchezaji huyo akirejea katika ubora wake katika msimu ujao wa 2024/2025. Fati aliweka bayana katika mkataba wake wa kwanza wa kikazi na Barca mwaka wa 2019, na hatima yake ilionekana nzuri mwanzoni, akiweka historia ya kufunga mabao katika mechi alizoshiriki.

Hata hivyo, misimu iliyofuata ilikuwa giza na kuandamwa na majeraha.

Mnamo Novemba, mwaka 2020, Fati aliumia goti lake la kushoto na, baada ya upasuaji, alikuwa nje kwa miezi tisa.

Mnamo Januari, 2022, mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikaa nje kwa miezi mitatu kufuatia jeraha la misuli ya paja. Kabla ya majeraha kutatiza maendeleo yake, wadadisi walimsifu kama mmoja wa vijana walio na kipaji bora zaidi ulimwenguni.

Septemba iliyopita, Fati alitolewa kwa mikopo wa msimu mzima kwenda Brighton. Alionekana katika mechi 27 za Seagulls hao akifunga mabao manne. Hasa, alicheza jukumu muhimu katika ushindi wa kihistoria wa Brighton wa mashindano ya Ulaya, akifunga bao la pili katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Ajax wakati wa hatua ya makundi.

Hatua hii pia ilionyesha bao lake la kwanza kwenye Ligi ya Europa. Sasa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amerejea Hispania, ripoti za Juni mwishoni zilionyesha La Blaugrana hao walikuwa na nia ya kumtoa tena msimu huu wa joto, labda wa kudumu, kutokana na wasiwasi mkubwa juu ya rekodi yake ya majeraha.

Hata hivyo, ripoti ya gazeti la Mundo Deportivo inapendekeza mchezaji huyo hauzwi tena au kupatikana kwa mkopo.

# SINGIDA BS: TUMEPANGWA KUNDI LA KIFO KAGAME CUP

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Singida Black Stars ikisema timu yao imepangwa katika kundi gumu kuelekea michuano ya Kombe la Kagame, Coastal Union wao wamefurahia ratiba ya michuano hiyo itakayofanyika kuanzia Julai 9 hadi 21, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Coastal Union iko katika Kundi A na timu za Al Wadi ya Sudani, JKU FC (Zanzibar) na Dekefaha (Somalia), huku Singida Black Stars ikiangukia Kundi C lenye SC Villa ya Uganda, APR (Rwanda) na El Merriekh (Sudan).

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Ayoub Omari, amesema wamefurahishwa na droo hiyo, haswa kupangwa kwenye kundi ambalo wanalimudu.

„Kundi tumelipokea kwa mikono miwili, ni saizi yetu kabisa na tunalimudu, naahidi tutawapa Watanzania burudani, hakuna mashaka tumejiandaa na mashindano hayo.

Hiki ni kipimo kwetu kuelekea katika michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika, watu wataona tumejiandaa vipi kwenye michuano hiyo," alisema katibu hiyo.

Aliongeza tayari kikosi chao kimeingia kambini kujiandaa na michuano hiyo na akaahidi watafika mapema Dar es Salaam ili kupata muda wa wachezaji wake kupumzika kabla ya kinyang'anyiro hicho kuanza.

Naye Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, aliliambia gazeti hili wamepangwa katika kundi la kifo, hivyo wana kazi ya ziada.

„Kundi nimeliona, katika makundi yote letu ndiyo gumu, lakini tunakwenda kujiandaa ili kupambana. Ni kipimo sahihi kwetu kupima ubora na daraja letu kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu.

Kocha wetu Mkuu (Patrick Aussems), ameliona, na yeye ndiye aliyeshauri tushiriki kwa ajili ya kupanga mbinu zake na kuangalia aina ya wachezaji waliosajiliwa, ila ukweli hatuna matarajio makubwa kwenye michuano hii zaidi ya kuitumia kujenga kikosi," Masanza alisema.



Wasanii wakipiga ngoma ya asili ya Kisukuma ya Mwaginya wakati wa maandalizi ya Tamasha la Utamaduni na Utalii la Kanda ya Ziwa linalotarajiwa kuanza leo hadi keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM mkoani Geita. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mazoezi Twiga Stars yakolea

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema anafurahishwa na ushindani uliopo katika kikosi chake kinachojiandaa na mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya Tunisia na Botswana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime, alisema kila mchezaji anajituma kwenye mazoezi kwa sababu hakuna nyota ambaye ana uhakika wa namba ya kudumu kwenye kikosi cha kwanza.

Shime alisema hali hiyo inasaidia kuimarisha ubora wa wachezaji wake na anakuwa na kikosi kipana.

„Kila mchezaji anajituma na anaonyesha juhudi, mazoezii yanaendelea vizuri, tunaamini timu yetu inazidi kuimarika, ujio wa wachezaji wanaocheza soka la kulipwa unasaidia kuongeza uzoefu," Shime alisema.

Wachezaji walioitwa kujiandaa na mechi hizo za kirafiki ni Najat Abasi kutoka JKT, Asha Mrisho (Amani), Lidya Maximilian (JKT), Protasia Mbunda (Fountain Gate), Enekia Kasonga (Eastern flames), Julietha Singano (Mexico), Vailet Mwamakamba (Simba Queens), Anastazia Katunzi, Joyce Lema na Janeth Christopher wa JKT.

Wengine ni Ester Maseke kutoka Bunda, Diana Lucas (Ame SKF), Aisha Juma (Simba Queens), Stumai Athumani, Winifrida Gerald (JKT), Maimuna Kaimu (ZED ya Misri), Elizabeth Charles ( Alliance), Aisha Masaka (BK- Hacken), Oppa Clement (Besiktas), Clara Luvanga (Al Nasr- Saudi Arabia), Victoria Maselle (TopHat Soccer Academy -Georgia) na Malaika Meena kutoka Forest University ya Marekani.

Twiga Stars imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), ambayo yamesogezwa mbele na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hadi Julai mwakani.

## Fadluraghman atua nchini kumalizana na Simba

INATOKA UK. 24

cha msaidizi.

Klabu zingine ambazo amewahi kufundisha ni Orlando Pirates ya Afrika Kusini kama kocha Mkuu mwaka 2021 ambapo kabla ya hapo alikuwa msaidizi kwenye klabu hiyo kuanzia mwaka 2019 chini ya makocha watatu kwa nyakati tofauti, Zinnbauer ambaye wamekutana naye tena Raja Casablanca, Milutin Sredojevic ‚Micho', na kocha Rulani Mokwena, aliyetimuliwa hivi karibuni kwenye klabu ya Mamelodi Sundowns.

Wakati Simba ikijiandaa kumtangaza kocha huyo, jana mchana imemtambulisha, beki wa kati, Hamza, akitokea klabu ya Super Sports ya Afrika Kusini.

Mchezaji huyo ambaye alijiunga na klabu hiyo 2023 akitokea Namungo FC, aliwahi kuzichezea pia klabu za KMC na Mbeya City.

Ni mchezaji wa pili wa Kitanzania kutambulishwa baada ya Lameck Lawi, lakini ni wa tano katika ya wachezaji wapya ambapo wengine waliotajwa mpaka sasa mbali na hao ni Jushua Mutale, Steven Mukwala na Jean Charles Ahoua.

## Taifa Stars yapangwa kundi H kufuzu Afcon 2025

INATOKA UK. 24

Taifa Stars, mara kwa mara imekuwa ikipata bahati ya kucheza na DR Congo kwenye michuano mbalimbali ikiwamo ya kufuzu fainali ya Kombe la Dunia na fainali zilizopita za AFCON ambapo zote zilikuwa kundi moja.

Mara ya mwisho Stars kucheza dhidi ya Guinnea ilikuwa Januari 27, 2021, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 katika mechi za kusaka kufuzu AFCON.

Stars haijakutana na timu ya taifa ya Ethiopia kwa miaka tisa, ambapo mara ya mwisho ilikuwa Novemba 30, 2015 kwenye robo fainali ya CECAFA iliyochezwa Addis Ababa, timu hizo ziliitoka sare ya bao 1-1 kabla ya wenyeji kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3, kabla ya hapo zilikuwa wote kundi moja na zilicheza Novemba 28 mwaka huo huo ambapo zilitoka sare ya bao 1-1.

Wenyeji wenza wa Tanzania kwenye fainali za AFCON 2027, Kenya na Uganda nao wamepangwa kwenye makundi tofauti.

The Cranes, wapo Kundi Kundi K pamoja na timu za Sudan ya Kusini, Congo na Afrika Kusini, huku Harambee Stars ikiangukia Kundi J, ikipangwa na timu za Zimbabwe, Namibia na Cameroon.

Baada ya fainali hizo za mwaka 2025, Tanzania pamoja na Uganda na Kenya zitakuwa mwenyeji wa fainali hizo zitakazofanyika mwaka 2027.

Michezo
Nipashe Ijumaa Julai 5, 2024

**Madrid kumtambulisha rasmi Mbappé Julai 16**

UKURASA 21





# Kocha Fadluraghman atua nchini kumalizana na Simba

Kocha huyo msaidizi wa Raja Casablanca anakuja kuchukua mikoba ya Benchikha kuinoa timu hiyo kwenye....

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI klabu ya Simba jana ikimtangaza mchezaji mwingine mpya, Abdulrazack Hamza kutoka Super Spprts ya Afrika Kusini, Kocha msaidizi wa Raja Casablanca raia wa Afrika Kusini, Fadluraghman 'Fadlu' Davids ametua nchini kwa ajili ya kufanya makubaliano ya mwisho kabla ya kutwaa mikoba ya kuifundisha timu hiyo.

Taarifa zilizopatikana jana zinasema kuwa kocha huyo maarufu kwa jina la Fadlu Davids, ametua nchini na huenda akatangazwa rasmi leo au kesho kushika mikoba iliyoachwa wazi na Abdelhak Benchikha raia wa Algeria ambaye aliondoka kabla ya ligi kumalizika na timu kukaimiwa na Juma Mgunda.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema Davids ndiye kocha ambaye aliwavutia mabosi wa Simba na kuamua kumpa timu, huku vikao vikiendelea vya kuwapata wasaidizi wake kukamilisha benchi jipya la ufundi la klabu hiyo.

„Kocha wetu kama nilivyokwambia awali ni Davids, anaweza kutangazwa Ijumaa au Jumamosi kama mambo yatakwenda vizuri, kuhusu nani atamsaidia na watu gani watakuwa kwenye benchi la ufundi hiyo bado, ila kuna mazungumzo na kocha mwingine anaitwa Darian Wilken naye ni raia wa Afrika Kusini ambaye wameshawahi kuwa wote kwenye klabu ya Orlando Pirates na Raja Casablanca," alisema mtoa taarifa huyo

Kocha huyo, anatua Simba akiwa ametoka kuisaidia Raja Casablanca kutwaa Ubingwa wa Morocco ikimaliza na pointi 72, ambapo katika mechi 30 ilizocheza, ilishinda mechi 17, ilitoka sare mechi tisa na haikupoteza mechi yoyote akiwa chini ya Kocha Mkuu, Josef Zinnbauer, akizima ndoto za kocha wa zamani wa Yanga, Nasreddine Nabi kutwaa taji hilo akiwa na FAR Rabat iliyomaliza ya pili.

Davids alikutana tena na Nabi, Julai Mosi, alipoiwezesha Raja Casablanca kuifunga FAR Rabat mabao 2-1 kwenye fainali ya michuano ya 'Moroccan Throne Cup', ambayo kwa Tanzania ni kama Kombe la FA.

Kabla ya kuchukuliwa na Raja Casablanca, Davids alikuwa akiifundisha Maritzburg United ya Afrika Kusini, mwaka 2023 alikwenda katika klabu Lokomotiv Moscow ya Urusi na kuwa ko-

INAENDELEA UK. 23

# Stars yapangwa kundi H kufuzu Afcon 2025

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' itakutana na timu za Guinnea, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika mechi za kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) za mwaka 2025 zitakazochezwa nchini Morocco.

Katika droo iliyofanyika jana alasiri nchini Afrika Kusini, Tanzania imepangwa Kundi H, ambapo italazimika kumaliza kwenye moja kati ya nafasi mbili za juu katika michezo itakayofanyika baadaye mwaka huu ili kwenda nchini Morocco kwa ajili ya fainali hizo zilizopangwa kuchezwa Desemba 21 mwakani hadi Januari 18, 2026.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042